Jumamosi Januari 9, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580455
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**Gigy Money unalo dada!**

UKURASA 13

**Serikali** yatangaza kufanya msako mifuko ya plastiki

UKURASA 3



**RC aagiza** watumishi walionunua matofali ya hospitali wakamatwe

UKURASA 3

# Trafiki atiwa mbaroni tuhuma rushwa ngono

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**NBS: MFUMUKO WA BEI UMEONGEZEKA**

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imesema mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Desemba 2020...

UKURASA WA 5

**MAOFISA 'WASHTAKIWA' KWA NAIBU WAZIRI MAJI**

WENYEVITI wa Halmashauri za Wilaya ya Rungwe na Busokelo mkoani Mbeya, wamewashtaki...

**Vita dhidi ya utumikishaji wenye ulemavu yapamba moto**

UKURASA 4



Rais Dk. John Magufuli akishuhudia utiaji saini wa Mkataba wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Mwanza hadi Isaka mkoani Shinyanga (Km 341), kati ya Shirika la Reli Tanzania TRC kupitia Mkurugenzi Mkuu, Masanja Kungu Kadogosa na ubia wa kampuni mbili za Kichina, China Civil Engineering Construction Corporation CCECC na China Railway Construction Corporation Limited CRCC, kupitia Mtendaji Mkuu wa CCECC, Zhang Junle (kushoto), katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu ndogo ya Chato, mkoani Geita jana. **PICHA: IKULU**

# Magufuli abaini soko la mazao Tanzania China

UKURASA 2



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play
Download on the App Store

**MICHEZO** NTIBAZONKIZA, KAZE WANG'ARA TUZO VPL UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Sueiman Abdulla, akizungumza na viongozi wa vyama tisa vya kisiasa wakiwamo waliogombea urais wa Zanzibar, ofisini kwake Mtaa wa Vuga, Mjini Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JPM abaini fursa soko mazao Tanzania China

**Na Mwandishi Maalum,** CHATO

RAIS John Magufuli jana alikutana na kufanya mazungumzo na Mjumbe wa Baraza la Taifa na Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, akibainisha fursa ya soko la mazao ya Tanzania katika nchi hiyo ya Asia.

Mazungumzo hayo yalifanyika Chato mkoani Geita, na kufuatiwa na tukio la Rais Magufuli kushuhudia utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa (standard gauge) kwa kipande cha kuanzia Mwanza hadi Isaka kati ya Shirika la Reli (TRC) na Kampuni ya Ujenzi ya China Civil Engineering Construction Company (CCECC).

Kipande hicho ni cha tano katika mradi mzima wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa, ambacho kina urefu wa kilometa 341 na ujenzi wake unatarajiwa kukamilika Januari 2024 kwa gharama ya Sh. trilioni 3.0617 zinazotolewa na Serikali ya Tanzania.

Akizungumza baada ya kutiwa saini kwa mkataba huo, Wang Yi alipongeza Tanzania kwa juhudi zake za kujenga barabara na miundombinu mingine kama China ilivyofanya na kwamba hatua hiyo itaisaidia Tanzania kupiga hatua kubwa za kimaendeleo kama ilivyo kwa China.

Akirejea maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Xi Jinping, alipofanya ziara yake ya nchini na ikiwa ni ziara yake ya kwanza tangu kuchaguliwa kuwa Rais wa nchi hiyo, mjumbe huyo aliziagiza kampuni za China zinazofanya kazi za ujenzi nchini, kufanya kazi hizo kwa ubora na kwa maslahi ya Tanzania. Katika hotuba yake, Rais Magufuli aliishukuru China kwa ushirikiano wake na Tanzania katika masuala mbalimbali yakiwamo ya kiuchumi na alimhakikishia Wang Yi kuwa Tanzania itaendeleza na kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano huo kwa maslahi ya pande zote mbili.

Rais Magufuli alipongeza kampuni ya CCECC iliyoshinda zabuni ya ujenzi wa reli kati ya Mwanza na Isaka, akieleza matumaini yake makubwa kuwa kampuni hiyo itafanya kazi nzuri ya ujenzi.

Alimshukuru Rais Xi Jinping kwa kumtuma Mjumbe wa Baraza la Taifa na Waziri wa Mambo ya Nje, Wang Yi kuja nchini kuwasilisha ujumbe wake, na kwamba naye amemtumia Rais Xi Jinping ujumbe ukiwa na masuala muhimu matatu ya kuendeleza ushirikiano katika uchumi.

Masuala hayo ni kuomba ufadhili katika miradi miwili ya uzalishaji umeme katika Mto Rufiji na Mto Lumakali, na pia kujenga kilometa 148 za barabara kuu Visiwani Zanzibar.

Pia aliomba kupatiwa msamaha wa madeni yakiwamo deni la Dola za Marekani milioni 15.7 lililotokana na ujenzi wa reli ya TAZARA, deni la Dola za Marekani milioni 137 lililotokana na ujenzi wa nyumba za askari na deni la Dola za Marekani milioni 15 lililotokana na ujenzi wa kiwanda cha Urafiki - Dar es Salaam.

Rais Magufuli alisisitiza kuwa Tanzania na China ni ndugu na marafiki wakubwa ndiyo maana Tanzania imezipatia zabuni kampuni za China katika ujenzi wa miradi mikubwa ambapo katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kampuni za China zilizofanya kazi Tanzania zimelipwa zaidi ya shilingi Trilioni 21 (sawa na zaidi ya Dola za Marekani Bilioni 10) zilizotokana na kodi za Watanzania. Kiongozi huyo wa nchi alitoa wito kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa China kuja kuwekeza nchini, na pia China kununua mazao ya Tanzania ikiwamo chai, kahawa, pamba na korosho hasa ikizingatiwa kuwa China yenye idadi ya watu takribani bilioni 1.6, ni soko kubwa la bidhaa mbalimbali zikiwamo korosho ambazo wanahitaji zaidi ya tani milioni 700 kwa mwaka. Rais Magufuli pia aiwahakikishia wafanyabiashara na wawekezaji wa China kuwa kwa kuwekeza Tanzania, watajihakikishia soko kubwa la Afrika Mashariki lenye watu milioni 165 na soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yenye watu takribani milioni 500.

Mara baada ya kuwasili Chato juzi, Wang Yi alifungua Chuo cha VETA cha Chato na kuchangia Sh. milioni 350 kwa ajili ya kununua vifaa vya uvuvi na jana asubuhi, alitembelea na kujionea shughuli za uvuvi katika Mwalo wa Chato na kuchangia Sh. milioni 45 kwa ajili ya kuboresha Mwalo huo.

Wang Yi aliondoka nchini jana na kuelekea Ushelisheli ambako anaendelea na ziara yake.


MUCOBA BANK PLC
P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.
E-Mail: mucoba@mucobatz.com

**TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA (21) WA WANAHISA WA BENKI YA MUCOBA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba, Mkutano Mkuu wa ishirini na moja wa Wanahisa utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 30 mwezi wa Januari 2021 katika ukumbi wa **MAM** –uliopo **Mafinga Mjini** kuanzia saa tatu kamili asubuhi.

Ajenda ya Mkutano itakua kama ifuatavyo:

1. Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha Akidi ya Wajumbe
3. Kuchagua Mwenyekiti wa Mkutano
4. Kuridhia ajenda za Mkutano
5. Kuthibitisha Muhtasari wa kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 20 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 30.11.2019 na mkutano wa dharura uliofanyika tarehe 11.4.2020
6. Kupokea,kujadili na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 20 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 30.11.2020
7. Kupokea na kujadili taarifa ya Mwenyekiti wa bodi ya Wakurugenzi ya Mwaka 2019.
8. Kupokea na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mwaka ulioshia tarehe 31.12.2019
9. Kupokea na kujadili mapendekezo ya Mkaguzi huru wa hesabu za benki kwa mwaka 2019
10. Kupokea na kujadili gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31.12.2019
11. Kupokea na kuidhinisha pendekezo la Malipo ya wajumbe wa Bodi
12. Kuwasilisha taarifa kuhusu mashauri yahusuyo Benki
13. Kupokea na kuidhinisha uteuzi wa wakaguzi wa nje wa hesabu kwa mwaka 2020
14. Kufunga Mkutano.

Notisi hii imetolewa leo tarehe 09/01/ 2021

Mambo ya kuzingatia

1. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria Mkutano huu atatakiwa kufanya hivyo kwa gharama zake mwenyewe; na atatakiwa
2. Iwapo Mwanahisa anayeruhusiwa kuhudhuria Mkutano na kupiga kura, atashindwa kwa sababu zozote zile kuhudhuria Mkutano, ataruhusiwa kuchagua Mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata na kuzingatia taratibu na sheria za Kampuni.
3. Nakala za Makabrasha ya Mkutano zitapatikana pia kwenye ofisi yetu kuu iliyopo Mafinga- Iringa.

**KWA AGIZO LA BODI YA WAKURUGENZI**
**PHILIP RAYMOND PHANUEL**
**KATIBU - BODI YA WAKURUGENZI**


# Trafiki atiwa mbaroni tuhuma rushwa ngono

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Kilimanjaro, inamshikilia askari wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani, Peter Moshi, kwa tuhuma ya kuomba rushwa ya ngono, ili kushughulikia kesi ya mtoto aliyegongwa na pikipiki.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapo, Frida Wikesi, alisema kuwa awali askari huyo alikamatwa kwenye nyumba ya kulala wageni iliyoko Soweto, Manispaa ya Moshi.

Wikesi alidai kuwa, wakati makachero wa TAKUKURU wanamkamata, walimkuta tayari ameshavua nguo ili kutekeleza azma yake ya kupokea rushwa ya ngono.

Alisema lengo la kuomba rushwa hiyo ni ili kukamilisha taarifa ya uchunguzi wa ajali husika na kumpeleka dereva aliyemgonga mtoto huyo mahakamani kwa haraka.

"Askari huyo alikuwa akimsumbua mama wa mtoto kwa madai kuwa ili haki ipatikane, hana budi kumpatia rushwa ya ngono na alipokataa, shauri la kesi hiyo lilichelewa kupelekwa mahakamani," alisema. Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema mtoto huyo bado anaendelea na matibabu na uchunguzi utakapokamilika, hatua kali za kisheria zitachukuliwa ili kutokomeza matukio kama hayo mahali pa kazi.

Aliwataka watendaji kutekeleza wajibu wao katika kila kitengo bila kuomba rushwa yoyote, akionya kuwa hatua kali za kisheria zitachukulia dhidi ya yeyote atakayebainika.

Mkazi wa mjini Moshi, Lovenes Samwel, aliiomba serikali kufuatilia matukio kama hayo mkoani Kilimanjaro, akidai kuwa yamekithiri. Alisema dawati la jinsia na ndani ya Jeshi la Polisi na mabaraza ya ardhi ya mitaa na vijiji, yanakabiliwa na vitendo hivyo vya rushwa ya ngono.

Faustina Msofe, mkazi mwingine wa mji huo alisema: "Tunamwomba Rais aliangalie upya Jeshi la Polisi hasa katika kitengo cha dawati la jinsia maana kwa sasa limekuwa sehemu ya unyanyasaji kwa wanyonge badala ya kuwasaidia.

"Kama hauna pesa, hakuna haki, la sivyo utoe rushwa ya ngono. Tunamwomba sana Mheshimiwa Rais amulike eneo hilo, kuna matatizo."

HABARI KITAIFA




Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Ernest Kimaya (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana na kutoa tamko kupinga ukatili dhidi ya wenye ulemavu ikiwamo ombaomba, kutumiwa kama mtaji. Kushoto kwake, Godson Mollel, Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ualbino Tanzania (TAS) na Feliciana Mkude, Mwenyekiti wa Bodi ya SHIVYAWATA. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Serikali yatangaza kufanya msako mifuko ya plastiki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetangaza kufanya operesheni maalum baada ya siku 90 kuwabaini na kuwakamata wafanyabiashara, wasambazaji, wazalishaji na wanaotumia mifuko ya plastiki kama vifungashio.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, alitangaza kusudio hilo jijini hapa jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu matumizi ya vifungashio vya plastiki kama vibebeo vya bidhaa.

Alisema hatua hiyo inakuja baada ya hivi karibuni kujitokeza tatizo la matumizi ya vifungashio vya plastiki aina ya tubings visivyokuwa na sifa na hivyo kutokidhi matakwa yaliyowekwa na Shirika la Viwango (TBS).

"Vifungashio hivi kwa sasa vinazalishwa kwa wingi na kwa ukubwa mbalimbali na vimekuwa vikitumika kama mifuko ya kubebea bidhaa sokoni na kuleta dhana kuwa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku, imerudi kivingine kama vifungashio," alisema.

Ummy alisema mifuko hiyo imeanza kuzagaa kwenye mazingira ya mitaa na vijiji kwa kasi kubwa na hivyo kurudisha nyuma mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi chote cha kupambana na mifuko ya plastiki.

Alisisitiza vifungashio vinavyoruhusiwa katika matumizi mbalimbali kama vyakula, sekta ya kilimo, huduma za afya na usafi vinatakiwa kukidhi sifa mbalimbali.

Alizitaja sifa hizo kuwa ni viwe na unene usiopungua microns 30 kwa upande mmoja au 60 microns pande mbili, viwe na lakiri ikimaanishwa kuwa kifungashio kinatakiwa kifungashwe na anayefungasha bidhaa yake ili kuuza kabla ya kwenda sokoni.

Alibainisha kuwa viwe na alama ya mzalishaji au anayepakia bidhaa na alama ya ubora inayotolewa na TBS.

Alisema vifungashio hivyo vimekuwa vikitumika kama vibebeo vilivyozagaa madukani, sokoni na maeneo mbalimbali na kuwataka wasambazaji, wazalishaji na waagizaji kuacha mara moja kuvitumia.

"Kwa kuzingatia maombi ya wafanyabiashara wadogo ambao wana shehena ya vifungashio hivi na kwa kuwa serikali ya awamu ya tano inathamini mchango wao katika juhudi za kujiongezea kipato katika kupambana na umaskini, ninatoa kipindi cha siku 90 visiwapo sokoni," alisema.

Aliwatoa hofu wananchi kuwa hapatakuwa na uhaba wa vifungashio vinavyokidhi viwango baada ya kipindi hicho kwa kuwa kwa mujibu wa kanzidata ya TBS, wapo wazalishaji wa kutosha wa vifungashio kukidhi mahitaji nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Mafwenga, alisema kwa mujibu wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira, ni marufuku mifuko ya plastiki kuzalishwa na kutumika nchini.

Alisema kitendo cha kuzalisha au kuingiza nchini mifuko hiyo ni kosa na adhabu yake ni faini isiyopungua Sh. milioni 20 na isiyozidi Sh. bilioni moja au kifungo kisichozidi miaka miwili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja.

# RC aagiza watumishi walionunua matofali ya hospitali wakamatwe

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, ameagiza kukamatwa kwa watumishi 13 wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele mkoani humo ambao wametumia zaidi ya matofali 81,000 yaliyofyatuliwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya hospitali ya wilaya hiyo.

Homera alitoa agizo hilo juzi baada ya kutembelea na kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa majengo saba na kubaini kuwa matofali yaliyokuwa yamefyatuliwa yameuzwa kwa watumishi wa halmashauri ambao wanadaiwa zaidi ya Sh. milioni 13. Watumishi wanaodaiwa kuuziwa matofali hayo ni James Chawe, Ramadhani Masudi, Martine Maswago, James Kapongo, Adam Mabihya, Peter Nyamafu, Lengay Longoy, Dk. Mketo, Ignatus Kamande, Aidan Ngwando na Philemon Mahombo pamoja na wananchi Abdallah Soud na Fortunata Kabeja.

Homera alisema kitendo cha watumishi hao kuuziana matofali yaliyofyatuliwa chini ya kiwango inaonyesha ilikuwa mbinu ya kufyatua ili yauzwe na kununuliwa na watumishi wenyewe.

"Ninachoona hapa haya matofali yalifyatuliwa chini ya kiwango kwa makusudi ili baadaye watumishi wauziane. Sasa naagiza wote waliouziwa wakamatwe mara moja, watatolewa rumande mpaka walipe fedha hizo. Wasipolipa hawatatoka ndani," alisema. Mei 2019, Halmashauri ya Wilaya ya Mlele ilimpata mkandarasi wa kufyatua matofali, lakini yalifyatuliwa chini ya kiwango.

Kutokana na hali hiyo, Homera aliunda kamati kuchunguza ambayo ilitoa ripoti kuwa hayafai kwa ujenzi, hivyo kuyaweka pembeni, lakini baadhi ya watumishi waliamua kuyanunua kwa mkopo, lakini ni miaka miwili tangu wayanunue hawajalipa fedha hizo.

Wakati huo huo, Homera ameagiza kukamatwa kwa wazazi na walezi wote watakaowaficha watoto wenye ulemavu kwenda shuleni katika msimu mpya wa masomo unaoanza kesho kutwa.

Alitoa agizo hilo baada ya kukagua na kuangalia maandalizi ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza na darasa la kwanza awamu ya pili katika wilaya za Mlele na Nsimbo.

Alisema ziko taarifa baadhi ya wazazi na walezi kuwaficha watoto wenye ulemavu jambo ambalo linakwenda kinyume cha haki za watoto na haki za binadamu.

Mkuu huyo wa mkoa aliiviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha watoto wote 11,000 waliomaliza elimu ya msingi mwaka jana, wanajiunga na elimu ya sekondari katika shule walizochaguliwa na wengine kujiunga na vyuo mbalimbali vya ufundi mkoani humo.

# NBS: Mfumuko wa bei umeongezeka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imesema mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Desemba 2020, umeongezeka hadi asilimia 3.2 kutoka asilimia tatu kwa mwaka ulioishia Novemba 2020.

Imesema kuongezeka kwa mfumuko huo kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula ikiwamo nyama, samaki wabichi, mayai, dagaa, mafuta ya kupikia, matunda, maharage, nguo za kike na kiume na viatu.

Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii wa Ofisi hiyo, Ruth Minja, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu mfumuko huo.

Alisema kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba 2020 imeongezeka kidogo kulinganishwa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia Novemba 2020.

"Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Desemba 2020, kumechangiwa na baadhi ya bidhaa za vyakula kama nyama kwa asilimia 3.1, samaki wabichi asilimia 15.6, mayai kwa asilimia tatu, dagaa kwa asilimia 13.2, mafuta ya kupikia kwa asilimia 9, matunda kwa asilimia 16.9, maharage kwa asilimia 6.2, choroko kwa asilimia 12, viazi mviringo kwa asilimia 5.5 na mihogo kwa asilimia 13.5," alisema.

Alifafanua kuwa, baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizoongezeka bei kwa mwezi Desemba 2020 kulinganishwa na bei za Desemba 2019.

Alizitaja bidhaa hizo kuwa ni pamoja na nguo za wanaume kwa asilimia 3.9, nguo za wanawake kwa asilimia 3.3, viatu vya wanaume kwa asilimia 2.5, viatu vya wanawake asilimia mbili, gesi ya kupikia kwa asilimia 7.1 na mkaa kwa asilimia 12.3.

Hata hivyo, alisema kwa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa Desemba 2020 mfumuko wa bei umeongezeka hadi asilimia tatu kutoka asilimia 2.8 kwa mwaka ulioishia Novemba 2020.

Kuhusu wastani wa mfumuko wa bei wa taifa kuanzia Januari hadi Desemba 2020, Minja alisema umepungua kwa asilimia 3.3 kutoka asilimia 3.4 kwa mwaka 2019 huku wastani wa bidhaa za vyakula ukiongezeka hadi asilimia tano kwa mwaka 2020 kutoka asilimia 4.3 mwaka 2019.

Kuhusu hali ya mfumuko kwa nchi zingine, mkurugenzi huyo alisema kwa Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Desemba 2020, umeongezeka hadi asilimia 5.62 kutoka asilimia 5.33 kwa mwaka ulioishia Novemba 2020 huku Uganda mfumuko kwa mwaka ulioishia Desemba 2020 umepungua hadi asilimia 3.6 kutoka asilimia 3.7 kwa mwaka ulioishia mwezi Novemba 2020.

# Vita utumikishaji wenye ulemavu yapamba moto

**Na Waandishi Wetu**



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, akimchapa viboko mmoja wa vijana ambao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya kudhalilisha watu wenye ulemavu kuombaomba mitaani. **PICHA: MAKTABA**

VITA imepamba moto. Ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na msako mkali dhidi ya watu wanaowatumia wenye ulemavu kujipatia kipato unavyozidi kupamba moto, huku taasisi mbalimbali zikitoa matamko mazito.

Hatua hiyo inaonyesha kuwaibua watu, ikiwamo serikali katika lindi la usingizi mzito na kuanza kuchukua hatua stahiki dhidi ya watu hao waliowafanya watu wenye ulemavu kuwa fursa ya kujipatia fedha.

Siku chache zilizopita, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kinondoni chini ya mkuu wa wilaya hiyo, Daniel Chongolo, walifanya msako na kuwakamata watu wakiwa wamewaweka watu wenye ulemavu katika jengo moja ambao walikuwa wakiwatumikisha kama kitega uchumi kujipatia kipato.

Kutokana na kuibuliwa sakata hilo, vita imepamba moto sehemu mbalimbali huku taasisi mbalimbali, zikiwamo za haki za binadamu na vyama vya kutetea masuala ya wenye ulemavu, zikitoa matamko mazito ya kulaani vitendo hiyo.

**WENGINE WANASWA**

Ikiwa ni siku chache baada ya watu kadhaa kunaswa wilayani Kindononi, Dar es Salaam, kwa tuhuma hizo, Jeshi la Polisi Mkoa wa Morogoro, linawashikilia watu wanane wanaotuhumiwa kujihusisha na biashara ya kuwatumia watu wenye ulemavu kujipatia kipato.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, alisema jana kuwa watu hao walikamatwa kwenye operesheni iliyofanyika juzi na jana katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema watu hao walikamatwa jana majira ya saa 9 usiku katika nyumba ya kulala wageni ya Sharonalo, iliyoko Kata ya Mwembesongo, Manispaa ya Morogoro.

Alisema wakati askari polisi wakiwa doria kwenye nyumba hiyo, waliwakamata Grace Hamisi (23) na Grace Jackson (21), wote wakazi wa Msamvu wakiwa wamepanga katika nyumba hiyo, huku wakikusanya fedha mitaani na kumpatia mmiliki wa nyumba hiyo Sh. 7,000 kama sehemu ya ujira wake kila siku.

Kamanda Musilimu alisema watu hao wenye ulemavu walikamatwa wakiwa na pesa na baada ya kuhesabiwa zilibainika kuwa ni Sh. 1,565,600.

Alisema polisi walibaini kuwa watu hao wenye ulemavu walikuwa wamepanga na watu wengine wanne waliojitambulisha kama wazazi wao, huku akikutwa kijana mmojawapo kati ya wawili ambao inadaiwa hufanya kazi ya kuwasukumiza na baiskeli watu wenye ulemavu kwenda kuomba pesa mitaani.

Musilimu aliwataja waliokamatwa kwenye tukio hilo kuwa ni James Christian (35) mkazi wa Sume- Msamvu, Amos Mkinga (31), Martha Hamisi (29), Ester Seleman (32), Mwigulu Shigela (29) na Sharif Ramadhani (28) wote wakazi wa Msamvu, Manispaa ya Morogoro.

Watuhumiwa hao, kwa mujibu wa Musilimu, watuhumiwa hao wanaendelea kuhojiwa na watafikishwa mahakamani mara upelelezi utakapokamilika.

**SHIVYAWATA YALAANI**

Kutokana na kushamiri kwa vitendo hivyo, Shirikisho la Vyama la Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), limelaani kitendo cha baadhi ya watu kuwatumia wenye ulemavu kama mtaji wa biashara na kujiingizia kipato.

Limesema kitendo hicho ni kinyume na mikataba ya kimataifa iliyotiwa saini na nchi katika kuheshimu haki na utu wa binadamu.

Mwenyekiti wa SHIVYAWATA, Ernest Kimaya, akizungumza jana jijini Dar es Salaam na kutoa tamko la kikao cha Bodi ya Shirikisho hilo kilichofanyika juzi, alisema anasikitishwa na vitendo vya baadhi ya watu kujipatia maslahi binafsi kwa kuwatumia ombaomba ambao ni wenye ulemavu.

"Tunalaani vikali vitendo vya kikatili vinavyodhalilisha utu na kuvunja haki za binadamu kwa watu wenye ulemavu vinavyofanywa na watu wasio na chembe ya upendo, huruma kwa binadamu wenzao," alisema Kimaya.

Alisema wanaunga mkono juhudi za serikali hususan hatua alizochukua Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Watu Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, na Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Kinondoni kukomesha vitendo hivyo.

Kimaya alisema kutokana na suala hilo kuwapo muda mrefu, ufanywe uchunguzi kubaini mtandao mzima unaotumika ikiwamo kufilisi mali za walionufaika na vitendo hivyo.

"Tunatoa wito wa programu endelevu kwa wadau wote kuonyesha ushirikiano kulisaidia kundi la watu wenye ulemavu, nao waishi maisha yanayowajengea heshima katika jamii," alisema.

"SHIVYAWATA tunaendelea kuiomba serikali iharakishe matumizi ya Daftari la Kudumu la Watu Wenye Ulemavu, ili kila mmoja atambuliwe na kusajiliwa katika mtaa, kijiji wanapoishi kama inavyoelekeza Kifungu cha 23 cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu namba 9 ya mwaka 2010," aliongeza.

Sambamba na hilo, aliwakumbusha waajiri wote kuzingatia ajira za watu wenye ulemavu, kwa uwiano wa asilimia tatu kwa mwajiri anayeajiri kuanzia watu 20 na kuendelea, kwa mujibu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu.

Alisisitiza kuwa hatua ya serikali na wadau kuwajengea uwezo wa kielimu kupitia vyuo vilivyo na stadi maalumu kwa watu wenye ulemavu, kuwapa msaada nyumbani mwao na si barabarani kutaibua vipaji na tatizo la ombaomba kupungua.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ualbino Tanzania (TAS), Godson Mollel, alisema watu wenye ulemavu wakiimarishiwa shughuli zao, vitendo vya kuwatumia kibiashara vitakoma.

"Juzi tu hapa hapa Dar es Salaam, watu wenye ulemavu na ombaomba wamewekwa gesti wakitumiwa kibiashara. Waliobainika waadhibiwe hata kufilisiwa," alisema Mollel.

Mjumbe wa Bodi ya SHIVYAWATA, Felician Mkude, alisema ombaomba na watu wenye ulemavu, walikuwapo tangu dahari, kikubwa ni kuwalinda, kupewa utu na haki.

"Shirikisho likianzishwa mwaka 1992 lilipoanzishwa tumeendelea kuweka juhudi za kuboresha huduma za kundi hili. Pia mkataba wa kimataifa wa Watu wenye Ulemavu uliotoka Novemba mwaka 2006 nchi 170 ziliridhia ikiwamo Tanzania, ikiwamo sera za kiutekelezaji nchini," alisema Mkude.

**THBUB YATOA NENO**

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imetaka serikali kuendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo mbalimbali ili kubaini vitendo vya udhalilishaji dhidi ya watu wenye ulemavu vinavyofanywa na baadhi ya wananchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, baadhi ya wananchi wamekuwa wakiwatumia watu wenye ulemavu kwa kuwafanya ombaomba mitaani ili kujiingizia kipato.

Alisema watu hao wamekuwa wakifanyiwa vitendo vingi vya udhalilishaji

jambo ambalo halikubaliki kisheria, hivyo serikali inapaswa kukemea vitendo hivyo ili kuhakikisha jamii hiyo inakuwa usalama.

Jaji Mwaimu alisema vitendo hivyo ni kinyume cha haki za binadamu zilizoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja

na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010 ambazo zinasisitiza utu wa mtu kuheshimiwa.

"Tunaomba serikali kuendelea kuwachukulia hatua kali watu wanaofanya vitendo hivyo kila mtu anapaswa kuheshimwa," alisema.

Mwaimu alisema tume hiyo inaungana na serikali pamoja na wadau wote nchini kukemea vitendo vya udhalilishaji na unyanyasaji dhidi ya watu wenye ulemavu na inatoa rai vitendo hivyo vikomeshwe mara moja.

- **Imeandikwa na Christina Haule, MOROGORO, Christina Mwakangale, DAR, na Renatha Msungu, DODOMA.**

HABARI KITAIFA

# Takukuru yageukia rushwa ya ngono

**Na Richard Makore,** MWANZA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mwanza imeitaka jamii kutoa taarifa za rushwa ya ngono katika maeneo mbalimbali yakiwamo kazini, shuleni, vyuoni, nyumbani na sehemu zingine.

Akizungumza na Nipashe juzi kuhusu wanavyopambana na rushwa ya ngono, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Stenga, alikiri kuwapo tatizo hilo na kuitaka jamii kutoa taarifa.

Stenga alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, wameanzisha dawati maalum la kupokea malalamiko na kuyafanyia kazi kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa Stenga, taarifa zilizopokewa kwao ambazo zinahusiana na rushwa ya ngono ni tatu na kwamba zingine zimefikishwa mahakamani.

Alisema kati ya kesi hizo za kuomba rushwa ya ngono, moja ilimkumba mwalimu wa shule ya msingi ambaye alishtakiwa na kuhukumiwa jela miezi 12. Stenga alisema lengo la kuanzisha dawati hilo ni kuhakikisha kunakuwa na uwazi katika kutoa taarifa za rushwa ya ngono kwa kila mtu anayefanyiwa vitendo hivyo.

Katika kuongeza nguvu katika suala hilo, Stenga alisema wamekuwa wakitoa semina mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wengine wakiwamo Taasisi ya Sauti ya Wanawake Ukerewe (SAWAU).

Wadau wengine wanaoshirikiana kutoa elimu hiyo kuhusu madhara ya rushwa ya ngono ni pamoja na The International Good Samaritan Mission for Improvement and Boosting Organizational Services to the Community, na MIBOS juu ya madhara ya rushwa ya ngono kwa vijana wa sekondari na vyuo.

Pia alisema jumla ya vipindi vya redio vinne viliandaliwa na kurushwa hewani kwa kushirikiana ili kuhakikisha elimu inawafikia walengwa.

Aliongeza kuwa waliandaa onyesho la siku moja katika siku ya wanawake duniani, ili kutoa elimu kwa wanawake na mabinti kuhusu madhara ya rushwa ya ngono kwa jamii.

Alifafanua kwamba tatizo la rushwa ya ngono lilizungumzwa katika semina 469 kwa wilaya zote za Mkoa wa Mwanza ili kufikisha ujumbe kwa jamii.



Mfanyabiashara wa masanduku ya kuhifadhia nguo akiyapanga vizuri kusubiri wateja wa kununua katika Soko la Vetenari Tazara jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Maofisa maji 'washtakiwa' kwa waziri

**Na Thobias Mwanakatwe**

WENYEVITI wa Halmashauri za Wilaya ya Rungwe na Busokelo mkoani Mbeya, wamewashtaki kwa Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, watumishi wa mamlaka za maji kwamba wanakula mishahara bure kutokana na kukaa ofisini tu.

Wamedai kuwa hatua hiyo imewafanya kushindwa kutatua kero za maji zinazowakabili wananchi katika halmashauri hizo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busokelo, Anyosisye Njobelo, na mwenzake wa Halmashauri ya Wilaya Rungwe, Mpoki Mwankuga, walisema hayo jana kwa Naibu Waziri Mahundi, ambaye alitembelea miradi ya maji katika halmashauri hizo.

"Hii ya watumishi kukaa ofisini kula mishahara bure hatutaki. Wapangiwe ratiba mara ngapi wanakwenda 'field' siyo wanakaa ofisini, wanasubiri mishahara tarehe 31," alisema Njobelo.

Njobelo alisema viko vyanzo vingi vya maji Busokelo, lakini cha kushangaza wananchi hawapati maji na hiyo ni kwa sababu watumishi katika idara ya maji si wabunifu wa kazi na badala yake wanakaa tu ofisini kusubiri mishahara.

Alitoa mfano kuwa kuna chanzo cha maji kilijengwa eneo ambalo silo na sasa maji hayatoki, hivyo wanataka fedha na hii inatokana na wataalam wakati mwingine kutosikia ushauri wa wananchi wa maeneo husika.

Naye Mwankuga alisema taarifa alizopewa Naibu Waziri wa Maji kuhusu hali ya upatikanaji wa maji si sahihi kwa sababu wao wanakaa na wananchi na wanaona wanavyopata kero ya maji.

"Mfano Mheshimiwa Naibu Waziri umeelezwa mradi wa Masoko unatoa maji wakati si kweli. Vijiji viwili havina maji. Pia umeelezwa kuwa zaidi ya vituo 300 vinatoa maji wakati si kweli, ukweli ni kwamba vituo hivi havitowi maji," alisema.

Mwankuga alisema Katibu Mkuu na Waziri wa Maji walifika wilayani Rungwe na kutoa maagizo kukamilika kwa miradi, lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika hali inayoonyesha kuwa wataalamu wamezoea kupewa maagizo na hawayatekelezi.

Kutokana na madai hayo, Naibu Waziri aliagiza mradi wa maji wa Masoko kufikia Februari 28, wananchi wawe wameanza kupata maji.

# Viongozi ushirika matatani tuhuma za kutafuna fedha

**Na Mwandishi Wetu,** CHAMWINO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Chamwino imeagizwa kuwachunguza viongozi wa Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Zabibu (CHABUMA AMCOS), kwa tuhuma za kutumia Sh. milioni 150 kinyume cha utaratibu.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Naibu Waziri Kilimo, Hussein Bashe, alipokuwa akizungumza na wawakilishi wa wakulima waliokusanyika katika shamba la zabibu katika kijiji cha Mwegamile wilayani hapa.

Bashe alisema kutokana na tuhuma hizo, viongozi hao lazima wachunguzwe na hatua stahiki zichukuliw.

Kuhusu uzalishaji katika shamba hilo, Bashe alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Umwagiliaji kupeleka wahandisi kuanzia jana ili washirikiane na wahandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kufanya tathmini ya gharama ya miundombinu ya umwagiliaji na kuiwasilisha mara moja kwake.

Pia aliagiza timu hiyo ya wahandisi kufanya tathmini kama mradi huo huo unaweza kutumia nishati ya jua katika kuendesha mashine za kuvuta maji yanayotumika katika kilimo cha umwagiliaji katika shamba hilo.

Bashe aliagiza kila mkulima ahakikishe ndani ya siku 30 anasafisha kipande cha shamba lake ndani ya shamba hilo, huku Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) ikiagizwa kufanya tathmini ya idadi kamili ya miche ambayo itahitaji kwa ajili ya kupandwa baada ya sehemu kubwa ya miche mingi kufa.

"Nakuagiza Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuandaa mafunzo ya namna ya kuendesha Ushirika imara na endelevu kwa Wakulima wa CHABUMA AMCOS ndani ya siku 30 kuanzia leo (jana)," alisema.

Awali, wakulima hao walimweleza Bashe kuwa CHABUMA AMCOS ilipokea fedha hizo kutoka kwa Kampuni ya ARCO Vintage mwaka jana kwa lengo la kuboresha miundombinu ya sehemu ya shamba hilo ili kampuni hiyo iendelee kununua shehena ya zabibu.

Hata hivyo, walisema viongozi wao walitumia fedha hizo kwa mambo mengine kinyume na utaratibu.

Walisema mwaka 2017 uzalishaji wa zabibu katika shamba hilo uliendelea kushuka na kusababisha wakulima kutelekeza mashamba yao na uzalishaji kusimama kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo adhabu ya riba kutoka Benki ya CRDB kuongezeka.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Namungo muda wa kupambana umefika

**KWANZA** tunapenda kutoa pongezi kwa wawakilishi wa Tanzania ambao wanashiriki katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba ya jijini Dar es Salaam kwa kufanikiwa kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Simba iliyokuwa chini ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck (ameachana na timu hiyo juzi), pamoja na nahodha wa zamani wa timu hiyo, Suleiman 'Veron' Matola imetinga hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuifunga FC Platinum kutoka Zimbabwe jumla ya mabao 4-1.

Hii ni baada ya kupoteza katika mchezo wa kwanza uliochezwa ugenini Harare kwa kufungwa bao 1-0, lakini Jumatano iliyopita ikatoa kipigo kitakatifu cha magoli 4-0, kwa wapinzani wao kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

Kwa matokeo hayo, Simba imeungana na timu nyingine 11 kutoka katika nchi mbalimbali barani Afrika kucheza hatua ya makundi, baada ya msimu uliopita wa mashindano hayo kutolewa mapema na UD Songo ya Msumbiji.

Mbali na Simba, wawakilishi wengine wa Tanzania waliobakia kwenye michuano hiyo ya kimataifa ni Namungo FC kutoka mkoani Lindi ambayo pia imefanya vyema kwa kuwaondoka Al Hilal Obeid ya Sudan kwa jumla ya mabao 5-3.

Namungo iliwafunga Wasudan hao mabao 2-0 katika mechi ya kwanza hapa nyumbani na ikalazimishwa sare ya mabao 3-3 walipokuwa ugenini jijini Khartoum.

Mechi hizo zimemalizika na sasa hivi Simba na Namungo zinatakiwa zijiimarishe kuelekea hatua inayofuata katika michuano hiyo inayosimamiwa na kuandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Simba na Namungo zinatakiwa kupitia mapema ripoti zao za kiufundi na kutumia muda mdogo wa usajili uliobakia kuimarisha vikosi vyao ili watakaposhuka tena uwanjani wawe tayari kushindana na si kushiriki kama ilivyozoeleka.

Usajili mzuri na utakaofanyika kwa malengo, utazisaidia timu hizi mbili kuwa na vikosi imara ambavyo vitatoa matokeo mazuri na hatimaye nchi kuweka rekodi ya kushinda mataji hayo yanayowaniwa na wawakilishi wetu hao.

Timu hizi mbili zitakapokuwa na vikosi imara, zitajiweka kwenye nafasi nzuri ya kupata matokeo chanya katika michezo yake iwe nyumbani au ugenini na kulitangaza vyema jina la Tanzania kwa upande wa soka.

Umefika wakati, timu za Tanzania zinapopata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa zikaogopewa kila zinapoonekana kwenye michuano hiyo na kamwe zisiwafanye wapinzani wao kuwaona 'ni wa kawaida'.

Inafahamika wazi katika mchezo wa soka hakuna kutegemea miujiza, inaeleweka ili timu yao ivune matokeo mazuri ni lazima wahusika wakubali kuwekeza kwa kufanya usajili wa kiwango cha juu, kuandaa programu sahihi ya kambi pamoja na kuwapatia wachezaji mahitaji yao yote muhimu.

Mataji au mafanikio yoyote kamwe hayapatikani kwa miujiza bali hutua kwenye timu iliyojiandaa vyema kuanzia hatua ya mwanzo wa msimu au ile iliyotumia vizuri kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Kuendelea kufanya vyema kwa klabu hizi, kutaihakikishia zaidi Tanzania nafasi ya kuwakilishwa na timu nne kwenye michuano hiyo kwa sababu ya idadi ya pointi itakazovuna.

Hakuna kisichowezekana, timu hizi mbili zinatakiwa kuendelea kujipanga kwa sababu hatua ambayo wamefika ni muhimu na kila klabu inahitaji kufika huko.

Viongozi wasiangalie wanatakiwa kutumia kiasi gani, wawekeze kuimarisha vikosi vyao kwa sababu mwisho wa siku, watavuna neema kupitia zawadi itakayotolewa na CAF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Ndugu chungu jirani mkungu

**NDUGU** huwa kama chungu lakini jirani ni kama mkungu, yaani mfuniko wa chungu unaotengenezwa kwa udongo. Methali hii hutumiwa kutukumbusha ndugu huwa na uhusiano wa karibu sana kuliko mtu na jirani yake.

Aidha, "Udugu wa nazi ni kukutana chunguni." Hutumiwa kuwapigia mfano watu wasioweza au wasiopenda kushirikiana hadi inapokuwa wakati mbaya sana na wanapochelewa. Yafaa kuitambua faida ya kushirikiana mapema.

'Chuki' ni hisia ya kutopenda kitu au jambo. 'Chukia' ni kitendo cha mtu kutopenda mtu mwingine au kitu. 'Chukiza' ni kitendo cha kufanya jambo la kuudhi. Kitendo cha kiumbe kufika kiwango cha kutopendeza kwa wengine kutokana na matendo yake.

Kwa hiyo ni dhahiri kuwa "Chuki humchoma anayeihifadhi." Kwa hiyo chuki humsumbua mno mtu anayeiweka au kuihifadhi. Methali hii yatufunza umuhimu wa kutoiweka chuki kwa kuwa tunajidhuru wenyewe.

'Mchezo' ni jambo ambalo watu au timu hufanya kwa kushindana ili kupata mshindi; jambo ambalo mtu hufanya ili kupitisha wakati au kujifurahisha wao na watazamaji.

Kabumbu, soka au kandanda ni mchezo wa mpira wa miguu aghalabu uchezwao kwa dakika 90 au zaidi kwa mujibu wa kanuni na unapendwa zaidi duniani. Kwa maneno ya mitaani, mchezo huo una jina refu: 'Gozi la ng'ombe; nyama kala nani.'

Ndio maana Mwalimu Nyerere (Mungu amrehemu), baada ya Tanganyika kuwa huru kutoka himaya ya Waingereza, alisema wananchi wote ni ndugu.

Kwa msisitizo imara, imani ya Chama cha TANU (Tanganyika African National Union) ambacho sasa chaitwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimeweka wazi kila mtu anastahiki heshima, kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.

Je, imani hiyo ya chama tawala ambayo yatakiwa ifuatwe na kutekelezwa kwa dhati bila unafiki, inafuatwa na kutekelezwa itakiwavyo au imebaki kwenye maandishi tu?

Yanga iliyoundwa mwaka 1935 na Simba mwaka uliofuatia, ndizo timu za kandanda zenye mashabiki wengi ndani na nje ya nchi. Hata hivyo hufanyiana vitendo vya hila, kila moja ikifanya hivyo dhidi ya nyingine!

Udugu ni uhusiano wa watu unaotokana na uzawa mmoja. Kwa maana hiyo, Tanzania. Pamoja na ukweli huo, Yanga na Simba zimekaliana kwa kile kiitwacho 'mguu-kausha' kila moja ikiwa adui wa nyingine!

Timu za nchi moja, mkoa mmoja, mtaa mmoja katika jiji moja la Dar es Salaam ambalo zamani liliitwa 'Bandari ya Salama' lakini zafanyiana uhasama wa kila aina. Kuchukiana, kufedheheshana, kuaibishana, kuchekana na kuzomeana hasa mojawapo inaposhindwa na timu ngeni ya ughaibuni.

Wahenga walisema "Ndugu chungu jirani mkungu." Maana yake ndugu huwa kama chungu lakini jirani ni kama kifuniko cha chungu. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa ndugu huwa wana uhusiano wa karibu sana kuliko mtu na jirani yake.

Badala ya Yanga na Simba kuwa mfano mzuri kwa timu zingine nchini, zimejenga uadui mkubwa baina yao. Pukachaka! (neno lenye kuashiria kutema mate ambalo humaanisha kukidharau kitu kilichotajwa.

"Msi kucha kwambwa nyamba." 'Kwambwa' ni kusemwa ilhali 'nyamba' ni mtu duni au wa kudharauliwa. Maana yake asiyeogopa kusemwa afanyapo jambo fulani ni mtu duni. Twakumbushwa umuhimu wa kuyafikiria na kuyawazia maoni ya watu wengine hasa tufanyapo jambo linaloweza kutuaibisha.

Viongozi wa Yanga na Simba wanapaswa kukutana ili kuwaeleza wanachama wao maana ya udugu. Zinapopambana na timu ngeni waache tofauti na ubozi (upumbavu) wao. Zishangilie timu za nyumbani.

Kufanyiana ubaya twajidhuru wenyewe kwani hata timu ngeni zinatufanya mazezeta yaani watu wenye matatizo ya akili; punguani.

Wanachama na mashabiki wa Yanga na Simba kuzishangilia timu ngeni ni kuwaonyesha wageni ujinga wetu wa kutojua maana ya bendera ya taifa letu inayopepea wakati klabu zetu zinapopambana na wageni hao.

Hii ni chuki ya kutotaka maendeleo ya Yanga na Simba mpaka kuwa na wivu wa kijinga na kusema: "bora timu ngeni ishinde ili jiji litulie; vinginevyo hatutalala usingizi kwa nderemo (hoihoi)!"

Isemwapo hivyo, wageni wakisikia hutucheka na kutudharau kimya kimya kwa umbumbumbu wetu, yaani watu wenye ufahamu mdogo wa mambo!

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 344 096**

## HABARI KITAIFA

# Mvua yakosesha makazi kaya 75

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

KAYA 75 katika Kijiji cha Lyapona Kata ya Kaengesa, Sumbawanga mkoani Rukwa, zimeachwa bila makazi baada ya mvua kubwa iliyonyesha ikiambatana na upepo mkali kubomoa na kuezua nyumba zao.

Pamoja na mvua hiyo iliyonyesha juzi mchana kuezua nyumba 15 na kuwakosesha makazi wananchi hao, pia imejeruhi watu watano ambao walipelekwa katika Kituo cha Afya cha Kaengesa kwa matibabu.

Mbunge wa Kwela, Deus Sangu, ambaye alifika eneo la tukio na kutoa msaada wa unga na sukari kwa waathirika, alisema mvua hiyo ilianza kunyesha saa 8:00 mchana na ilinyesha kwa zaidi ya saa mbili, hivyo kusababisha maafa hayo.

Alisema baada ya kutokea kwa maafa hayo, waathirika waliomba hifadhi kwa ndugu, jamaa na marafiki wakati wakisubiri utaratibu mwingine kutoka mamlaka zinazohusika.

"Kwa sasa tunaendelea na kazi ya kuokoa mali mbalimbali na baada ya hapo tathmini ya maafa hayo itafanyika kujua uharibifu uliojitokeza. Lakini kimsingi tunahitaji msaada wa kibinadamu kwani hali ni mbaya," alisema.

Sangu aliwataka wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kuacha tabia ya kukata miti ovyo kwa kuwa athari zake ni pamoja na maeneo mengi kuwa jangwa, hivyo inapotokea kimbunga au upepo mkali, nyumba nyingi huathirika kwa kung'oka paa na kusababisha maafa.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Dk. Halfan Haule, alikiri kupokea taarifa ya maafa hayo na kueleza kuwa bado kamati ya maafa inaendelea kufanya tathmini ya maafa hayo.

Katika kipindi cha mwezi mmoja sasa, zaidi ya nyumba 130 zimeezuliwa paa na zingine kubomoka kabisa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani Rukwa.

Maeneo yaliyoathirika na mvua hizo ni vijiji vya Malonje, Malagano katika Manispaa ya Sumbawanga, Kinambo na Lyapona kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Sumbwanga.




Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (katikati), akimsikiliza Mkuu wa Kikosi cha Polisi Wanamaji nchini, ACP Evance Mwijage (kulia), akimwonyesha waziri huyo maeneo mbalimbali ya ukanda wa Bahari ya Hindi wanayofanyia kazi, walipokuwa ndani ya boti ya polisi kuona utendaji kazi wa kikosi hicho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

# Naibu Waziri akumbana na madudu urasimishaji ardhi

**Na Munir Shemweta,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameshangazwa na halmashauri za mkoa wa Kilimanjaro kuingia mikataba ya urasimishaji na kampuni nane ambazo zimeshindwa kukamilisha kazi, hivyo kusababisha kuanza kuchunguzwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU).

Akizungumza jana na uongozi wa mkoa wa Kilimanjaro, wakurugenzi wa halmashauri, watendaji wa sekta ya ardhi na kampuni za urasimishaji katika ofisi ya mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Mabula alisema haiwezekani wakurugenzi wote wa halmashauri kuingia mikataba na kampuni zaidi ya nane za urasimishaji katika mkoa na kushindwa kukamilisha kazi.

"Wakurugenzi wote mko hapa wakati mnaingia mikataba na kampuni hizi mlizichunguza kabla ya kuingia mikataba? Maana haiwezekani mkoa mzima kampuni zishindwe kukamilisha kazi kwa wakati. Naagiza halmashauri zifanye uchunguzi kabla ya kuzipa kazi kampuni," alisema.

Dk. Mabula alisema kampuni za upimaji hazitakiwi kwenda kinyume cha mpango uliowekwa na halmashauri na zinatakiwa kufanya kazi kwa kwenda mtaa kwa mtaa na si mtu kwa mtu. Pia alisema halmashauri zinatakiwa kuzichunguza na kuchukua zile zenye uwezo na mtaji badala ya kutegemea fedha za wananchi.

Aliiagiza Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango Miji na Kampuni kuzichunguza kampuni zote za urasimishaji ambazo hazijakamilisha kazi na wakibaini kampuni zisizo na uwezo, zifutwe kufanya tena kazi ya upangaji na upimaji nchini.

Naibu Waziri aliongeza kuwa wizara iliona jambo jema kushirikisha sekta binafsi katika urasimishaji kwa lengo la kuongeza kasi ya upimaji na kusisitiza kuwa inachotaka ni kampuni inayopewa kazi ni kuwa na angalau asilimia 50 ya mtaji kwa ajili ya kazi husika badala ya kutegemea fedha za wananchi.

"Wizara inasema kama huna fedha usitegemee pesa za wananchi kuendesha kazi ya urasimishaji na tusiwafanye wananchi mtaji kwa kuwa mwisho itakuwa kero kwa kushindwa kukamilisha kazi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa KILI Surveys Ltd, Alphonce Mwanshinga, alijitetea mbele ya Naibu Waziri kuwa kampuni yake tayari imeshapima viwanja 2,795 na kulipwa Sh. milioni 283,361,000 huku ikiendelea kudai Sh. milioni 247,639,000 kutoka kwa wananchi.

Alisema kikwazo kikubwa kwa kampuni yake kushindwa kukamilisha kazi hiyo kwa wakati ni kuwa walipoanza kazi waliendesha urasimishaji kulingana na mwitikio wa wananchi na kuamua kupima kwa wale waliolipa fedha.

Hata hivyo, alisema kampuni yake inatarajia kukamilisha upimaji katika mtaa waliopewa mwisho wa mwezi huu.

Kampuni zilizopewa kazi ya urasimishaji kwenye mkoa wa Kilimanjaro, mbali na KILI Surveys Ltd, ni Makazi Solution, E&M Contruction Ltd, Land Surveys and Consultancy Services na EM Land Consultants.

# DC apiga 'stop' michango wanafunzi

**Na Yasmine Ptotace,** MKURANGA

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga, Filbeto Sanga, amewataka walimu kutowatoza michango ya aina yoyote wanafunzi ambao wanaoanza shule.

Sanga aliyasema hayo jana katika kikao maalumu cha Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, kilichoitishwa kubadilisha matumizi ya fedha ili ziende kutumika katika ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule 10.

Ujenzi wa madarasa hayo utawawezesha wanafunzi 3,627 ambao mwaka huu walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, lakini wakabakizwa kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, kuanza masomo.

"Nitoe onyo kwa walimu ambao watapokea wanafunzi waache kuwatoza michango na ambaye atakamatwa akifanya hivyo, atachukuliwa hatua za kisheria," alisema.

Pia Sanga aliongeza kuwa agizo la serikali la kutaka ifikapo Februari 28, mwaka huu, wanafunzi waliofaulu wawe wameripoti, alisema Mkuranga imeshaanza kufanya taratibu za kuongeza vyumba vya madarasa katika baadhi ya shule.

"Niwashukuru madiwani kwa kukubali kupitisha fedha za matumizi kupeleka katika ujenzi wa vyumba ya madarasa ili wanafunzi waendelee na msomo yao," alisema.

Sanga aliongeza kuwa ujenzi utafanyika kwa kuongeza majengo katika shule ambazo nafasi zipo.

Kwa mujibu wa Sanga, wanafunzi 7,329 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, lakini kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa, watoto 3,700 ndio waliojiunga lakini wengine 3,627 wamebaki kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

# Kortini kuendesha gari njia ya mwendokasi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Pwani, limemkamata na kumfikisha mahakamani dereva wa kampuni ya mabasi ya Happy Nation, kwa tuhuma za kuendesha gari la abiria kwa njia za hatari.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alimtaja dereva huyo kuwa ni Jahian Madeni (44), mkazi wa Mbezi Luis jijini Dar es Salaam, aliyekuwa akiendesha gari lenye namba za usajili T.617 DTK aina ya Yutong.

Wankyo alisema tukio hilo lilitokea Januari 5, mwaka huu, wakati gari hilo likitokea Dar es Salaam kwenda Morogoro.

Alisema basi hilo ilipofika eneo pacha la ujenzi, Kibaha, kituo cha mabasi, dereva aliendesha kwa njia za hatari katika barabara kuu ya Morogoro.

Alisema mwendo huo ulisababisha taharuki kwa watumiaji wengine wa barabara hiyo.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Wankyo ametoa onyo kwa waendeshaji wa vyombo vya moto wanaopitia Pwani kuendesha magari kwa umakini na kufuata sheria za usalama barabarani.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akimsikiliza Mhandisi Raphael Laizer kutoka Tume ya Umwagiliaji Dodoma ambaye alikuwa akitoa maelezo ya namna ya kuifanyia ukarabati miundombinu ya umwagiliaji wa matone katika shamba hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vifo ajali barabarani vyapungua 25%

**Na Christina Haule,** MOROGORO

VIFO vinavyotokana na ajali za barabarani mkoani Morogoro vimepungua kutoka 90 mwaka 2019 hadi 57 mwaka jana, sawa na asilimia 25.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, alisema jana kuwa vifo hivyo vimepungua kutokana na elimu inayoendelea kutolewa kila wakati kwa madereva wa malori, mabasi, teksi, wanafunzi na magari binafsi.

Alisema mwaka 2019, ajali 75 zilitokea na kati ya hizo, 67 zilisababisha vifo 90 na majeruhi wakati mwaka jana, ajali 54 zilitokea na kusababisha vifo 57 vilivyotokana na ajali 37 kati ya ajali zilizotokea.

Kamanda Musilimu katika kuhakikisha ajali hizo zinapungua, Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa, lilitoa elimu kwa abiria wa mabasi 3,600, madereva 2,000 wa pikipiki, wanafunzi 4,000 kwa kila mwezi mkoa mzima kutokana na kuweka vipindi maalum vya elimu ya usalama barabarani shuleni na kwa madereva wa magari binafsi na daladala wapatao 3,600 kila mwezi.

Alisema ajali hizo zimesababishwa na magari binafsi, pikipiki, malori makubwa na magari ya abiria, ambapo chanzo kikiwa ni madereva kushindwa kumudu magari, kuacha njia na kupinduka kunakosababishwa na usingizi unaotokana na uchovu hasa kwa madereva wa malori.

Kamanda Musilimu alivitaja vyanzo vingine vya ajali hizo kuwa ni kutaka kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari, vitendo ambavyo hufanywa mara kwa mara na madereva wa magari binafsi na pikipiki pamoja na ulevi na uendeshaji magari mabovu.

Aidha, kamanda huyo alisema wanaendelea na operesheni za kila siku barabarani kwa ajili ya kutoa elimu ya masuala ya usalama barabarani na kuwataka madereva kufuata sheria huku wakizidi kuimarisha operesheni na kuwapima madereva ulevi.

Alisema madereva wamekuwa wakipimwa kipimo maalum cha kutambua kama wamelewa pombe au la kwenye vituo mbalimbali vya barabara ikiwamo stendi za mabasi wakati wanataka kutoka kwenye vituo vya mabasi na maeneo ya mizani.

Dereva wa gari binafsi, Dafrosa Archard, alisema baadhi yao huona kusubiri gari lililo mbele liende naye aende, huwa shida na pia hushindwa kuzingatia sheria kwa kusubiri gari la upande mwingine lipite ili naye apite hasa pale gari lingine linapopaki mbele yake likiwa bovu.

Naye Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa wa Morogoro, Mrakibu Mwandamizi (SSP) Michael Stephen, aliitaka jamii kushirikiana vyema na polisi ili kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa ajali za barabarani.

Pia Stephen aliwataka abiria kuzingatia uvaaji mikanda wawapo kwenye magari ambayo alisema husaidia kupunguza vifo kwa abiria pale ajali inapotokea.

"Mara nyingi ajali ikitokea wale wasiofunga mikanda huwa ndio wa kwanza kupata madhara makubwa na pengine kupoteza maisha kwa sababu hutupwa huku na huko na gari. Takwimu zinaonesha gari likipata ajali, madhara makubwa na vifo hutokea kwa wasiofunga mikanda," alisema Stephen.

# Wasajili wa NGO wakumbushwa kuhusu wajibu wao

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, ametaka uwajibikaji, uzalendo na maadili ya utumishi wa umma kwa maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri na mikoa ambao kisheria ni wasajili wasaidizi wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO).

Maofisa hao kwa mujibu wa sheria, ndio wasimamizi wa usajili na uratibu wa NGO katika ngazi za mikoa na wilaya.

Dk. Jingu aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo kwa wasajili wasaidizi wa mashirika yasiyo ya kiserikali kwa mkoa wa Arusha yenye lengo la kuwajengea uwezo na uelewa wa namna bora ya kusajili na kuratibu mashirika hayo katika maeneo yao.

Alisema wasajili wasaidizi hao wanatambulika kisheria, hivyo wanataka kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa wakizingatia kuwa wamebeba dhamana kubwa ya kumsaidia Msajili wa NGO kutambua na kuhakiki mashirika hayo kabla ya kusajiliwa.

"Tuhakikishe tumatimiza wajibu wetu. Tumechaguliwa kuifanya hii kazi basi tuwe waadilifu, wazalendo na tuzingatie maadili ya utumishi wa umma katika kuyatekeleza majukumu yetu," alisema.

Dk. Jingu aliongeza kuwa uwapo wa wasajili wasaidizi wa NGO katika mikoa na halmashauri kunasaidia serikali kutambua mashirika yanayotekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kutatua matatizo na kuwaletea wananchi maendeleo.

Mwakilishi wa Msajili wa NGO, Mussa Leitura, aliwasihi wasajili wasaidizi hao kumsaidia Msajili wa NGO katika usajili na uratibu wa mashirika hayo kwa ngazi walizomo.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Arusha, Blandina Nkini, alisema mafunzo hayo yatawasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao ya kumsaidia msajili wa NGO katika hatua za awali za usajili na uratibu wa mashirika hayo katika utekelezaji wa miradi.



# Ummy ageukia halmashauri ukusanyaji taka

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Ummy Mwalimu, ameziagiza halmashauri nchini kuwa na mfumo bora wa ukusanyaji, kuhifadhi na kusafirisha taka ili kulinda afya za wananchi.

Ummy alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ziara ya kushtukiza kwenye Soko Kuu la Majengo jijini Dodoma kwa lengo la kuangalia mfumo mzima wa kushughulikia taka ngumu.

Katika ziara hiyo akiwa ameambatana na watendaji kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira, Waziri Ummy alionyesha kuridhishwa na hali ya mazingira sokoni hapo ya uhifadhi, ukusanyaji na usafirishaji hatua ambayo ameipongeza Halmashauri ya Jiji kwa kazi hiyo.

Akizungumza na watendaji, viongozi wa soko na wafanyabiashara wa soko hilo, alizitaka halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatoa kandarasi kwa watu wa kukusanya na kusafirisha taka wenye vifaa bora na wanaokidhi vigezo.

Ummy alisisitiza kuwa kutafanyika ukaguzi kote nchini kwenye halmashauri na miji kuona kama makandarasi hao wana vigezo na sifa zikiwamo kuwa na vifaa vya kuwakinga wafanyakazi wanaokusanya taka.

"Tumeona magari ya kukusanya na kusafirisha taka yenyewe yakiwa ni takataka. Kwa hiyo tutakagua kila halmashauri na miji ili wajitathmini, je, kandarasi hii waliyompa mtu wa kukusanya, kuhifadhi na kusafirisha taka ana vifaa bora na anakidhi vigezo," alisisitiza.

"Hizi ni salamu tu tunataka masoko yote yawe safi na salama kwa wanaouza na wateja, kikubwa ninasema mazingira safi na salama kwa ajili ya maendeleo endelevu," aliongeza.

Alitaka kuwapo kwa utaratibu wa kuondoa taka zinazokusanywa na kuhifadhiwa kwenye masoko kwa wakati na kwamba hatavumilia kuona halmashauri yoyote ambayo takataka zinakaa kwa zaidi ya siku moja.

"Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake inazitaka halmashauri zote za majiji, manispaa, miji na wilaya kuweka mifumo bora ya kukusanya, kuhifadhi na kusafirisha taka ngumu," alisema.

Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, alisema kuna tatizo la kupotea kwa vifaa wanavyokabidhiwa vibarua hali ambayo imekuwa ikisababisha ukusanyaji wa taka kutofanyika kwa wakati.

Alisema pamoja na kasoro hiyo, Jiji litaendelea kutoa vifaa hivyo ili kuliweka katika mazingira yaliyo safi na ubora kwenye masoko yote yaliyoko ndani ya halmashauri hiyo.

Naye Ofisa Afya wa Kata ya Majengo, Yusta Maguzu, alimhakikishia Waziri Ummy kuendelea kusimamia ukusanyaji, uhifadhi na usafirishaji wa taka ili mazingira ya soko yawe safi na bora kwa matumizi ya wateja na wafanyabiashara wake.



Mbunge wa Jimbo la Hanang', mkoani Manyara, Mhandisi Samwel Hhayuma, akizungumza na wananchi wa eneo hilo, juu ya mikakati ya maendeleo na kupambana na changamoto juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mtafiti ataka kuku kuuzwa kwa uzito

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAFUGAJI wa kuku wametakiwa kuuza kwa kupima kwenye mizani badala ya kukadiria ili kufanya biashara yenye tija.

Mtafiti Mwandamizi wa Mifugo, Mary Mwangoka, kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) Kituo cha Mpwapwa, aliyasema hayo juzi katika ziara ya waandishi wa habari na watafiti iliyoandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Mwangoka alisema wafugaji wengi wamekuwa wakiuza kuku kwa makadirio ya uzito jambo ambalo linasababisha kupata faida kidogo, hivyo ni wakati sasa wafugaji hao kubadilika ili kujiinua kiuchumi.

"Kuuza kwa makadirio kunafanya biashara ya kuku kuwa ngumu. Wakitaka kufurahia soko lazima wafanye biashara ya kupima kuku kabla ya kuwauza," alisema Mwangoka.

Alisema katika sehemu ambayo itafanya wafugaji wa kuku kufurahia soko ni pale wanapouza kwa kuzingatia uzito.

"Unakuta kuku wengi huuzwa kati ya Sh. 8,000 hadi Sh. 10,000 kwa makadirio, lakini kuku huyo unakuta anauzwa Sh. 15,000 na kuendelea akifika sokoni fedha ambayo alitakiwa kupata mfugaji," alisema.

Mwangoka alisema katika utafiti uliofanywa kwa kuhusisha kuku 157, umegundua ya kuwa endapo jogoo (kuku) atapimwa urefu wake kwa kutumia futi, kunaweza kukadiria uzito halisi, pia kuku jike atapimwa kwa upana wake atakadiriwa kwa uzito wake halisi.

Mwangoka alisema wafugaji wanapaswa kuzingatia vipimo hivyo, ambavyo vitasaidia wafugaji kupata njia rahisi ya kukadiria uzito halisi wa mifugo yao, badala ya mizani, ambayo ni gharama kubwa.

"Tunaiomba serikali iweke utaratibu wa kuuza kuku wa nyama kwa kupima kilo halisi ili wafugaji waache kunyonywa na madalali, bali wapate thamani sawa ya biashara wanayofanya," alisema Mwangoka.

## Ujenzi daraja waanza rasmi

**Na Augusta Njoji,** KONGWA

SERIKALI imeanza ujenzi wa daraja la Chamkoroma linalounganisha Wilaya za Mpwapwa na Kongwa ambalo lilisombwa na maji na kusababisha kuwapo na adha ya usafiri kwa wananchi.

Daraja hilo lipo ndani ya barabara ya Pandambili-Mlali -Mpwapwa hadi Ngh'ambi inayojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.1 na kampuni ya Bahati Investment.

Akizungumza jana katika ziara yake ya kukagua maeneo yaliyoharibiwa na mvua katika Wilaya ya Kongwa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alimtaka mkandarasi kujenga njia ya mbadala ndani ya siku mbili ili wananchi watumie wakati ujenzi wa daraja ukiendelea.

"Daraja hili ni muhimu sana katika kukuza uchumi wetu, kuharibika kwake kumezuia shughuli za kiuchumi kwa wananchi kuendelea. Niwapongeze Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) Mkoa wa Dodoma kwa usimamizi, lakini niwaombe mumsimamie mkandarasi huyu ili akamilishe kwa wakati na njia mbadala isizidi siku mbili iwe imekamilika," alisema.

Dk. Mahenge aliwasisitiza TANROAD kumsimamia mkandarasi ili daraja lijengwe kwa kiwango kulingana na thamani ya fedha iliyotolewa ili kukamilika kwa muda uliowekwa.

"Wekeni muundo ambao wataalamu mtaridhika nao. Unapojenga kitu kisichokuwa na ubora haikudumu na baada ya muda fulani kinaharibika, hivyo kuzuia fedha ambazo zingetumika kwingine. Naomba mjiridhishe na kile ambacho kitafanyika hapa ili kiwe cha uhakika," alisisitiza Dk. Mahenge. Aliwashauri pindi wanapoanza mradi wowote wakae na wenyeji wa eneo husika, ili kupewa historia ya eneo na hivyo kuepuka kurudia kufanya kazi mara mbili endapo itaharibika.

"Wataalamu jiongezeni, mkandarasi anapotekeleza mradi wowote lazima ujiulize sana endapo kuna mvua na vitu vingine, ndiyo maana tunasema unapofika kwenye eneo pata historia ya eneo husika, mnapokwenda 'kudesign' bila kujua chochote cha eneo hilo ndio inatokea muda mfupi mradi unaharibika," aliongeza.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serera, aliwakumbusha wananchi suala la upandaji wa miti ili kuzuia wingi wa maji unaoharibu miundombinu ya barabara.

"Hivi karibuni nilifanya kikao hapa na kuhimiza suala la utunzaji wa mazingira ili kuokoa miundombinu yetu, tukipanda miti kwa wingi maji yanayopita hapa hayatakuja kwa kasi hadi kupelekea uharibifu wa miundombinu," alisema Dk. Serera.

Akizungumza katika ziara hiyo, Kaimu Meneja wa TANROAD Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Salome Kabunda, alisema wanachofanya kwa sasa ni kuona namna ya kuzuia maji ili yasiharibu zaidi wakati huu ambapo kazi inaendelea.

"Kazi hii tunayoifanya ipo kwenye uwezo wa mkandarasi na ndani ya wiki tatu au mwezi mmoja mkandarasi ameahidi kukamilisha daraja hili, na tuahidi kuwa tutamsimamia ili akamilishe kwa wakati," alisema.

Awali, Diwani wa Chamkoroma, Saimon Binde, alisema tatizo lililopo ni uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanywa na wananchi. "Hapa kuna wananchi wamejimilikisha ardhi mlimani huko, wanalima wanafanya uharibifu wa kukata misitu na hivyo kumaliza misitu iliyopo na kupelekea eneo hili kwa kiasi kikubwa kuharibiwa na mvua," alisema.



# Maalim Seif ataja jitihada kuboresha huduma za kifedha

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inaendelea kufanya jitihada za kuboresha huduma za kifedha kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Amesema jitihada hizo zina lengo la kuondoa vikwazo mbalimbali kwa wananchi na kuifanya Zanzibar kuwa na huduma nzuri za kifedha.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa jengo jipya la PBZ, Malindi Mjini Unguja ikiwa ni miongoni mwa shamrashamra za kuadhimisha miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Maalim Seif alisema kumekuwa na vikwazo vingi kwa wateja wanaotumia benki hiyo ikiwamo msongamano.


Maalim Seif alisema katika kutatua hilo, jengo hilo litasaidia katika kuboresha huduma za kibenki na kuwaondolea usumbufu wananchi.

Alisema kuwa hatua hiyo ni kubwa kimaendeleo katika mji wa Zanzibar hasa Mji Mkongwe ambayo pia itawasaidia wafanyakazi wa benki kufanya kazi katika mazingira mazuri, hivyo kutoa huduma bora na kwa ufanisi kwa wateja.

Alisema ufunguaji wa matawi mbalimbali ya PBZ katika maeneo tofauti ya Tanzania, utarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wajasiriamali, wakiwamo wavuvi, wakulima na wafanyabiashara wadogo pamoja na kuwawezesha kupata mikopo ili kujiendeleza kiuchumi.

"Serikali yetu inatambua juhudi ambazo Benki ya Watu wa Zanzibar inazifanya katika kuwafikia wananchi na kutoa huduma bora ili kukidhi matakwa ya wananchi kwa kuendelea kufungua matawi mengine na vituo mbalimbali vya kutoa huduma," alisema.

Pia alisema PBZ ilioyanzishwa miaka 55 iliyopita, ni miongoni mwa taasisi kongwe za kifedha Tanzania zilizoanzishwa kwa lengo la kutoa huduma za kuwakomboa wananchi katika sekta zote za kiuchumi, hivyo katika kutimiza miaka 57 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, serikali inapenda kuiona inatimiza malengo yake.



Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, akihutubia wananchi na wageni waalikwa katika uzinduzi wa jengo la P.B.Z huko Malindi Mjini Zanzibar katika shamra shamra za miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# Mwinyi azionya polisi, mahakama kuhusu rushwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameziitaka polisi, mahakama na hospitali kujitathimi kuhusu rushwa na kuhakikisha zinaondokana na tuhuma dhidi yao kuhusu vitendo hivyo.

Amesema rushwa ni miongoni mwa mambo yanayokwaza utoaji haki katika vyombo vya sheria na taasisi zinazotoa huduma na kuzitia doa taasisi hizo.

Dk. Mwinyi alisema hayo juzi katika mkutano uliofanyika kwenye Ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni Zanzibar kujadili masuala ya ukatili wa kijinsia na namna ya kukabiliana nao.

"Tusipopambana na rushwa hili jambo litakuwa gumu. Naitaka ZAECA (Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) kuongeza bidii. Wakati mwingine wala si rushwa, ni urasimu tu, lazima tutafute njia ya kuondoa urasimu," alisema.

Alisema takwimu zilizowasilishwa na watoa mada katika mkutano huo zinatia shaka kutokana na kuwapo idadi kubwa ya kesi ambazo watuhumiwa wameachiwa.

Ili kutokomeza ukatili wa kijinsia, alishauri kuundwa kamati maalum itakayowashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo ambalo limeshamiri katika jamii.

Alisema kutokana na ukubwa wa tatizo la udhalilishaji lililoshamiri nchini, kuna umuhimu wa kuunda kamati maalum itakayowashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo polisi, mahakama na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na kufanya kazi kulingana na hadidu rejea ili kulipatia ufumbuzi tatizo hilo.

Dk. Mwinyi alisema miongoni mwa majukumu ya kamati hiyo yatakuwa kufuatilia kesi zilizoko mahakamani, kuangalia haja ya marekebisho ya sheria, uimarishaji wa maeneo ya kupima waathirika wa matukio ya udhalilishaji, kuimarisha madawati ya Polisi pamoja na matatizo yatokanayo ya taasisi za kidini katika eneo la ufundishaji, kama vile madrasa.

Suala la udhalilishaji, alisema ni kubwa na limekuwa likiitia aibu nchi pamoja na kuleta maumivu makubwa kwa waathirika, hivyo akataka itambulike kuwa ni vita vya kitaifa, hivyo kila mmoja mahali alipo atapaswa kutoa ushirikiano ili kumaliza tatizo hilo.

Dk. Mwinyi alisema ni wakati mwafaka wa kuangalia mitaala ya skuli pamoja na kufanya tathmini kwa madrasa zilizopo baada ya kuwapo taarifa kuwa baadhi ya walimu kutuhumiwa kuhusika na vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanafunzi, lakini baada ya kufukuzwa huanzisha vyuo vyao.

Alisema ni wakati sasa kwa Wizara ya Afya kuimarisha sehemu za upimaji wa waathirika wa ukatili wa kijinsia pamoja na kuwa na vifaa vya kazi vya kutosha, ili jamii iondokane na usumbufu.

Aidha, aliitaka Idara ya Mahakama kuondokana na mkwamo katika usikilizaji wa kesi unaochukua kipindi kirefu, hatua aliyosema inawachosha walalamikaji wa kesi hizo.

# Asifu ushirikiano vyama na serikali

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema utayari uliyoonyeshwa na viongozi wa vyama vya siasa kushirikiana na serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi wote umeleta faraja kubwa.

Alisema utayari huo unaokwenda sambamba na azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuendelea kutekeleza wajibu wake ndani ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, utaongeza kasi ya uwajibikaji kutoka kwa viongozi wa serikali na taasisi za kisiasa.

Hemed alisema hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa vyama tisa vya siasa wakiwamo waliogombea urais wa Zanzibar kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka jana.

Viongozi hao wa kisiasa walifika ofisini kwa Makamu wa Pili wa Rais kwa lengo la kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika kasi yake ya kuimarisha uchumi na ustawi wa jamii.

Alisema mchango na mawazo ya viongozi hao katika kujenga nchi, hauna mjadala kwa vile unatoa fursa pana zaidi ya kuimarisha umoja na mshikamano kwa vile unatoa nafasi kwa kila mwananchi kuwa na haki na wajibu wa kutoa mchango wake.

Aliwathibitishia viongozi hao kuwa serikali itaendelea kutoa ushirikiano wakati wowote katika kuona huduma za kijamii zinawafikia watu wote na pale inapotokea athari ndani ya utekelezaji huo, ni vyema ikaripotiwa panapohusika.

Kuhusu amani, alisema mchango wa viongozi wa kisasa ni muhimu katika kusimamia tunu hiyo ya taifa pamoja na usalama wa nchi.

"Kuna kila sababu kwa viongozi wa vyama vya siasa kuendelea kusimamia suala la amani na utulivu kutokana na kuwa na sauti na mvuto wa kukubalika na jamii ninayowazunguka," alisisitiza.

Aliwapongeza viongozi wa vyama vilivyoshiriki uchaguzi mkuu kutokana na umahiri wao uliosababisha vuguvugu la kisiasa Zanzibar kumalizika ndani ya muda mfupi baada ya kumalizika kwa mchakato huo.

Hemed alisema kwa vile maisha baada ya uchaguzi yanaendelea, ni vyema kila mwananchi akaendelea kutekeleza wajibu wake, huku akiwataka wawe na subra katika kipindi hiki ambacho Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, anaendelea kuchukua uamuzi mgumu katika kujenga nchi.



ANATISHA!

# Diamond kinara kutazamwa Afrika

ANATISHA! Ndivyo unavyoweza kumwelezea mwanamuziki maarufu wa Tanzania, Diamond Platnumz, baada ya kuwabwaga wasanii wakali wa Afrika kwa kuongoza nyimbo zake kutazamwa na watu wengi.

Katika orodha moya iliyotolewa na mtandao wa You tube, Diamond amekuwa kinara baada ya wimbo wake wa Jeje, kutazamwa na watu milioni 41.1.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, msanii wa muziki wa Bongo Fleva na CEO wa lebo ya WCB, amepotsi orodha ya nyimbo 10 ambazo mtandao huo unaelezea ndio nyimbo zilizotazamwa zaidi katika Bara la Afrika.

Katika orodha hiyo, nyimbo zingine za Diamond ambazo zimeshika nafasi ya juu ni 'Waah' namba tatu na Gere aliyoimba na mzazi mwenzake Tanasha Donna, ambayo ipo nafasi ya saba.

Nafasi ya pili imechukuliwa na Simi kutoka Nigeria kupitia wimbo wake Duduke, ambao umeangaliwa na watu milioni 29.

Diamond aliwashukuru mashabiki wake kwa kuandika "kwasababu ya upendo wenu mmeniwezesha kuiwakilisha vyema nchi yetu na kupata Most viewed song 2020, lakini hata kwa wimbo tulio utoa ndani ya muda mfupi tu HYPERLINK "https://www.instagram.com/explore/tags/waah/" #WAAH kushika nafasi ya 3... Hii inaonesha ni kiasi gani muziki wetu unazidi kukua."

Nyimbo zingine ambazo zimeingia katika orodha hiyo ni 'Noboddy' wa Dj Naptune akishirikana na wasanii Joeboy na Mr Eazi kutoka nchi za Nigeria na Ghana.

Vibration ulioimbwa na Rireboy kutoka Nigeria umeshika namba tano, huku Rayvanny kutoka WCB amekuwa nafasi ya sita kupitia wimbo wake 'Teamo' uliotazamwa na watu milioni 22.4.

BASI SAWA

## Barakah umelianzisha, utalinywa mwenyewe

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Barakah The Prince, ameweka pilipili katika kidonda kibichi, baada ya kudai asilimia 85 ya muziki ni kelele na fujo.

Msanii hiyo, amewapaka wenzake kwamba wanapoimba wanataka wimbo usikike tu, bila kuangalia wazo na maudhui yake.

"Nimejaribu kupitia baadhi ya nyimbo mpya zimetoka hivi karibuni, nimegundua asilimia 85 ya miziki hiyo ni kelele nyingi, miziki iliyokosa topic yaani fujo fujo tu bora usikike, tunapaswa kujitafakari wanamuziki wa kizazi hiki cha nyoka," amesema Barakah The Prince.



## Shamsa kama utaweza utampa raha

MWIGIZAJI mkongwe wa filamu za Bongo Muvi, Shamsa Ford, ameanza mkakati wake wa kupunguza mwili ili kuwa na mwonekano utakaomfurahisha mpenzi wake mpya.

Shamsa Ford amesema anataka kufanya mazoezi ya kupunguza uzito angalau kilo 25 ambazo zitamsaidia afya yake kuwa imara na mwonekano wa kuvutia.

"Nimekumbuka kaumbo kangu, huu mwaka ni mazoezi sana na diet, nataka kukata kilo 25 na nitaweza kwa ajili ya afya yangu pia kwa ajili ya 'my honey' nisije nikaonekana shangazi yake bure, 2021 mwonekano mpya," ameandika Shamsa Ford katika ukurasa wake wa Istagram.





## Duh! Rose Ndauka kapata mume

MUME wa mwingizaji mkongwe nchini, Rose Ndauka, anayejulikana kwa jina la Haffiyy Mkongwa, anataka mke wake kuzaa mapacha ili wafikie haraka idadi ya watoto anaowataka.

Akizungumza na EATV, Mkongwa amesema kwa sasa wana mtoto mmoja, anasubiria mpaka atakapofikisha miaka miwili ndiyo waongeze wengine.

"Tunashauriwa na serikali na vyombo vingine mbalimbali vya kiafya kwamba mtoto afikishe angalau miaka miwili ndiyo muweze kupata mwingine ila binafsi nitangoja mpaka akue kabisa na kujitambua, nataka watoto wengine wawili na ikiwezekana wawe mapacha ili tuweze kumaliza kwa haraka," amesema Haffiyy Mkongwa.



## Gigy Money unalo dada!

BAADA ya Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) kumfungia mwanamuziki wa Bongo Fleva, Gigy Money, kutojihusisha na masuala ya burudani na sanaa kwa muda wa miezi 6 pamoja na faini ya Sh. milioni 1, baadhi ya mashabiki wake wameongea mazito.

BASATA imetoa adhabu hiyo kufuatia tukio la msanii huyo kupanda jukwaani na kisha kuvua gauni lake na kubakia na nguo inayoonyesha maungo yake ya ndani.

Baada ya adhabu hiyo baadhi ya mashabiki wa muziki wameipongeza serikali na kusema msanii huyo anaongoza kwa matukio yenye utata ambayo yanaweza kuwashawishi watu kwenda kinyume na maadili.

"Gigy Money amekuwa akifanya mambo mengi yenye utata, kwa hili tunaipongeza serikali kuchukua hatua yeye kama msanii mkubwa anatakiwa kujitambua ili kuwa na taswira nzuri," amesema Amina Bundara.



## Wake walioimbwa na waume zao

**Na Adam Fungamwango**

KWA kizazi cha sasa si rahisi kusikia kuwa kuna msanii amemtungia nyimbo mkewe. Sana sana labda atamtungia mpenzi wake, halafu hataji jina vile vile. Labda ni kwa sababu ya kuepuka usumbufu.

Lakini wanamuziki wa zamani, pamoja na mambo mengine, walikuwa na sifa ya kuwatungia nyimbo wake zao. Hii iliwafanya waweke ndoa zao kwenye hali ya furaha na amani.

Leo hii inaonyesha jinsi wanamuziki wa zamani, mbali na kuimba mambo mbalimbali ya kiserikali, kichama, na matukio ya dharura yaliyokuwa yakijitokeza nchini, lakini walikuwa wakiwatungia nyimbo baadhi ya wanawake ambao walikuja kuwa wake zao, au kuwatungia wake zao.

Kwenye makala hii nitaanza na nyimbo ambazo wanamuziki waliwatungia wake zao kwenye miaka ya 1980 hadi 1990.

**DADA EMMY-MARIJANI RAJAB**

Mwanamuziki maarufu nchini Marijani Rajab ni miongoni mwa wanamuziki waliowahi kuwatungia nyimbo wake zao. Wimbo aliomtungia mkewe ni 'Dada Emmy'. Anamwambia mkewe kuwa yuko mbali na nyumbani ni kwa sababu ya kutafuta maisha. Anamsihi kuwa asibadili moyo wake na kumuacha anapata mateso kwani penzi lake kwake halina mfano. Duru zinasema kuwa Marijani alilazimika kutunga wimbo huo, baada ya msuguano fulani hivi uliotokana na wimbo wa 'Aisha'.

Ni wimbo ambao baadhi ya wambea walikwenda kumweleza mkewe kuwa alimtungia mpenzi wake ambaye anaishi Mwanza. Majirani baada ya kuweka mambo sawa, akaamua amtungie mkewe, mambo yakakaa sawa.

**ASHA MWANA SEIF-TX MOSHI WILLIAM**

Mwanamuziki Tx Moshi William inawezekana ndiye anayeongoza kwa kumtungia mkewe nyimbo nyingi kuliko mwanamuziki yeyote yule. Lakini wimbo maarufu ni 'Asha Mwana Seif'.

Ni wimbo ambao mume anamuuliza mama watoto kwa nini yuko kimya, mkewe anamwambia anatatizwa na tabia yake ya ulevi, huku watoto wakiwa wanateseka. Moshi na mkewe Asha Seif wote ni marehemu.

Kuna wimbo unaitwa 'Hamida', ukiwa wa kwanza kuutunga alipojiunga na Juwata Jazz Band akitokea Polisi Jazz, nao pia umhusu mkewe huyo huyo ambaye Hamida ni jina lake.

Vile vile Moshi alimtungia mkewe huyo huyo wimbo unaitwa 'Cheusi Magala'. Magala ni jina la kiasili la mkewe huyo aliyekuwa na asili ya Kinyamwezi.

**PAMELA-FRESH JUMBE**

Pia wimbo huu ulipigwa na bendi ya Juwata Jazz wana Msondo Ngoma. Mtunzi wa wimbo huu ni mwanamuziki Fresh Jumbe ambaye kwa sasa yupo nchini Japan, akiendelea na kazi yake ya muziki.

Aliutunga wimbo wa 'Pamela' ambaye ni mkewe, akisifu kwa wema aliumfanyia kuwa ni asili na yeye hata kama akiulipa utakuwa ni wa kuiga tu.

**MAMA FELLY-COSMAS CHIDUMUE**

Mwanamuziki huyu ambaye kwa sasa anapiga nyimbo za injili, aliutunga wimbo huu kwa ajili ya mkewe ambaye kwa sasa ni marehemu. Mtunzi anamwambia mama Felly maneno aliyoyasikia kwa majirani kama ana mpango wa kuoa mwingine si ya kweli.

**MARY MARIA-HEMED MANETI**

Kwenye wimbo huu wa 'Mary Maria', mtunzi wa wimbo huo, marehemu Hemed Maneti alimwimba mkewe kumweleza jinsi gani anavyompenda na kila anaposafiri anamfikiria yeye Maria, akaongeza kuwa hajapenda namna hii toka kuzaliwa na hatopenda mpaka siku ya kufa.

## Hukumu ya Penzi; chips kuku sumu tosha

**Na Adam Fungamwango**

KWA miaka mingi sasa, baadhi ya watoto wengi wa kike wamekuwa wakiacha masomo kutokana na mimba zisizotarajiwa.

Mabinti wa shule za msingi, sekondari na hata chuo, baadhi ya watoto wamekuwa wakipata ujauzito kutokana na tamaa na vitu vidogo vidogo vinavyoweza kuepukika.

Na moja kati ya vitu maarufu ambavyo vimekuwa vishawishi vya wanafunzi na chakula aina ya chips. Pamoja na kuwekwa sheria kali kwa pande zote mbili, kwa wanaowapa mimba wanafunzi, na hata wanafunzi wenyewe kuachishwa shule, lakini bado hali hii imekuwa ikiendelea, ingawa serikali imekuwa ikijitahidi kupambana.

Mtunzi wa filamu ya 'Hukumu ya Penzi' anawakumbusha wasichana kuwa makini na jambo hilo, kikubwa ni kuepuka tamaa za muda mfupi ambazo zinasababisha majuto ya milele.

Imechezwa na wasanii Tecla Yusuph, Luckey Luckamo, Hidaya Kitalile, Cindy Eda na wengine wengi.

Recha ni msichana anayefanya vema kwenye masomo yake ya kuchaguliwa kwenda chuo kusomea mambo ya biashara. Baba na mama yake wanajidhiki na kupata pesa kwa tabu kwa ajili ya kumsomesha binti yao.

Anapofika chuoni mambo yanabadilika. Rafiki yake Zamda anamwingiza kwenye janga la kumtafutia mwanaume, kwa sababu tu ni muuza chips.

Lengo ni kwamba kila ikifika mchana na usiku wawe na uhakika wa chakula wakiwa chuoni. Kweli, Recho anaanza mapenzi na kijana Mweleka.

Hatimaye anapata ujauzito ambao unamfanya kuacha masomo na kurejea nyumbani.

Simanzi inatawala nyumbani, hadi pale alipojifungua mtoto na kuomba tena arudishwe chuoni.

Baba wa mtoto alijitokeza eti lengo ni kutaka akae na mwanamke kwa ajili ya kulea mtoto, akatolewa baruti na wazazi. Baba alitoa tena pesa ya ada, binti akaenda kusoma. Huko alipata mchumba mwingine Dickson.

Huyu sasa haikuwa ya kishuleshule. Ilikuwa ya ukweli ya kupeleka barua amuoe. Hilo linafanikiwa.

Lakini ndoa inakuwa ndoana hadi anaachika. Hata hivyo alikuwa ameshamaliza masomo yake.

Recho, akaamua kuachana na mambo ya mapenzi. Badala yake akapata kazi na baadaye akaanza kufungua biashara zake.

Mambo sasa yakaanza kumwendea vizuri, akajenga bonge la nyumba kwao kiasi cha kumfurahisha na kumfuta machozi baba yake.

Recho sasa akawa amemaliza machungu yote ya mwanzo, lakini akawa anakumbuka nyuma jinsi chips zilivyomponza na kutimuliwa chuo kutokana na ujauzito.





# Kanye, Kim ndoa yao mashakani

RAPA mwenye mafanikio kutoka Marekani, Kanye West, na mkewe Kim Kardashian, wameanza kupata ushauri kuhusu namna ya kuokoa ndoa yao.

Kulingana na mtandao wa TMZ, wanandoa hao kwa muda mrefu hawapo katika maelewano kiasi ambacho wawili hao hawaishi katika nyumba moja kwa muda mrefu.

Vyanzo kadhaa vinasema ndoa hiyo ilikuwa katika matatizo makubwa katika nusu ya mwisho wa mwaka 2020 na hali hiyo inahatarisha kuvunjika kwa ndoa hiyo.

Imeelezwa katika muda huo Kanye West anaendelea kuishi katika nyumba yake iliyopo eneo la Wyoming, na Kim Kardashian, yupo Calabasas na watoto wake.



## Orisabunmi afariki dunia

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Folake Aremu, maarufu kama Orisabunmi, amefariki dunia akiwa na miaka 60.

Kifo chake kimethibitishwa na Rais wa Chama cha Sanaa na Upigaji Picha cha Nigeria, Bolaji Amusan, ambaye alisema msanii huyo alifariki Jumanne, lakini hakutaja chanzo cha kifo chake.


Orisabunmi, katika uhai wake amecheza filamu 80 ambazo zilionyeshwa kwenye televisheni na aliolewa na wanaume kadhaa ambao aliachana nao.

## Paul Okoye awa mwalimu wa covid-19

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Paul Okoye, anaendelea vizuri baada ya kupata matibabu ya ugonjwa wa Covid-19.

Nyota huyo wa muziki ambaye alikuwa mwanzilishi wa kundi la P square, amekuwa akijitenga baada ya kupata maambukizi ya virusi vya corona.

"Nawatakia heri ya mwaka mpya, nawaomba kuweni waangalifu na virusi vya corona, najua sio rahisi kwa Waafrika kuamini, lakini mimi nina uzoefu na mwalimu baada ya kuugua," ameandika.






## Mashabiki wamwombea Dr. Dre

MASHABIKI wa muziki wa Hiphop, wamekuwa na wasiwasi kuhusu afya ya Rap na mtayarishaji wa muziki Dr Dre, ambaye wiki hii amelazwa hospitalini kutokana na tatizo la ubongo.

Dr Dre (55) ambaye ana ushawishi mkubwa katika muziki nchini Marekani, alifikishwa katika Hospitali ya Cedarsili-yopo mjini Los Angelsnsiku ya Jumatatu, kulingana na mtandao wa TMZ.

Katika akaunti yake ya Instagram, nyota huyo alisema kwa sasa anaendelea vizuri baada ya kupata matibabu ya kiwango cha juu.

## Walinzi wa Stonebwoy matatani

WALINZI wawili wa msanii Stonebwoy, wametiwa mbaroni na polisi wa jimbo la Ashanti, baada ya kuendesha gari vibaya na kusababisha ajali.

Kwa mujibu wa polisi, imeelewa tukio hilo lilitokea tarehe Januari 2, mwaka huu katika barabara ya Bibiani-Abuakwa.

Kulingana na watoaji taarifa, Stonebwoy ana walinzi wake hao walikuwa wakirudi kutoka Bibiani, wakiwa ndani ya gari jeusi Toyota Land Cruisers, walikuwa wakiendesha kwa fujo na kusababisha ajali hiyo.



MAKALA

# UVAMIZI CAPITOL HILL



Waandamanaji wakipambana na polisi nje ya jengo la bunge.

## •Anguko ustawi demokrasia Marekani
## •Trump kubeba lawama ya tamaa

**Mwandishi Wetu**

JUMATANO ya Januari 6 itabaki kwenye kumbukumbu duniani kote, baada ya jengo la bunge la Congress ambalo linaheshimiwa nchini Marekani, kuvamiwa na kulazimika wabunge kutolewa mlango wa dharura.

Wavamizi hao ambao wameshtumiwa duniani kote, walikuwa na lengo moja tu, nalo ni kuhakikisha wabunge wanashindwa kumwidhinisha Joe Biden, kuwa Rais mpya wa nchi hiyo.

Nyuma ya watu hao yupo Rais Donald Trump, ambaye anaonekana kupinga matokeo yaliyompa ushindi Biden, akidai kulikuwapo na wizi wa kura.

Maelfu ya wafuasi wa kiongozi huyo, walivamia jengo hilo mjini Washington DC, na kuwashinikiza wabunge kutomwidhinisha Biden, ambaye anatarajiwa kuapishwa Januari 20 mwaka huu.

Siku hiyo asubuhi, Rais Trump, aliwahutubia waandamanaji wanaomuunga mkono kuwa hatambui ushindi wa Biden akiamini kulikuwa na wizi wa kura katika uchaguzi wa Novemba.

Aliwahamasisha kundi la watu ambao walizidi kuongezeka na kuimba kwa nguvu kwa kuwaambia wakomeshe wizi na vitendo vya kipuuzi.

Trump aliwashawishi watu hao kutembea kutoka Ikulu ya White House hadi jengo la bunge la Capitol Hill.

"Hatutarudi nyuma. Hatutakubali," Trump alisema.

"Nchi yetu haitakubali tena. Hatuwezi kuvumilia tena."

Aliongeza kwa sauti.

Wakati kiongozi huyo anamaliza kuzungumza na wafuasi wake ambao wote ni wazungu, ndani ya bunge wabunge walikuwa wakichuana vikali kuhusu kujumuisha matokeo ya kura ya wajumbe kutoka majimbo yote.

Hata hivyo, Makamu wa Rais, Mike Pence, alitangaza kumthibitisha Biden kuwa mshindi baada ya wabunge kumpigia kura.

Warepublican waliwasilisha ombi la kupinga ushindi huo, wakidai kura za Arizona zilkuwa na kasoro, lakini mabunge mawili ya wawakilishi na lile la seneti ziliitupilia mbali baada ya kuhakiki.

Kabla ya tukio hilo, vikao bungeni vilendelea kwa utaratibu huku pande zote mbili zikishangilia na maspika wao wakitoa matamko.

"Kiapo nilichokula Jumapili iliyopita kutetea na kuunga mkono Katiba kinanifanya niwajibike kupinga uovu huu," alisema mbunge mpya Lauren Boebert, ambaye amepata umaarufu baada ya kutangaza angeingia bungeni akiwa na bunduki. IMAGES

Ndani ya seneti, mjadala ulichukua mkondo mwingine. Kiongozi wa wengi katika Bunge la Seneti Mitch McConnell, aliyekuwa amevalia suti nyeusi sawa na ile ya kwenda mazishini, alikwenda kumzika Donald Trump, na sio kumsifu.

"Ikiwa huu uchaguzi ungelifutwa kutokana na madai ya upande ulioshindwa, demokrasia yetu ingelikuwa imeingia mzunguko wa kifo," McConnell alisema.

Kisha aliendelea: "Tusingeona tena nchi nzima ikikubali matokeo ya uchaguzi. Kila baada ya miaka minne tungelishuhudia jinsi watu waking'ang'ania madaraka kwa gharama yoyote."

Seneta wa Kentucky, ambaye atakuwa kiongozi wa wachache baada ya chama chake Republican kushindwa katika Jimbo la Georgia, amesema bunge lilibuniwa ili kokomesha matamanio ya muda mfupi ambayo yanaweza kuhujumu msingi wa nchi yetu".

Wakati akitoa matamshi hayo, kumbe nje ya bunge hali ilikuwa imebadilika, wafuasi wa Trump ambao huenda walikuwa wamehamasika na hotuba za awali, wakaamua kuvamia bunge.

Waandamanaji walipambana na maofisa wachache wa usalama waliyokuwa langoni na kisha wakaingia ndani ya bunge.

Vikao vilisitishwa ghafla huku wabunge, wafanyakazi wa bunge na wanahabari wakilazimika kujificha kwa kuhofia usalama wao.

Sarakasi iliendelea kushuhudiwa bungeni huku vituo vya televisheni vikionesha picha za waandamanaji wakicheza dansi nje ya jingo la bunge huku wakipeperusha bendera.

Picha za waandamanaji waliokuwa ndani ya bunge zilianza kusambazwa katika mitandao ya kijamii, baadhi yao wakijaribu kuvunja madirisha na kuingia katika ofisi za wabunge.

Maofisa wa usalama walionekana wakiwaelekezea bunduki watu waliotaka kuingia ndani ya Bunge la Wawakilishi.

**BIDEN AKATISHA HOTUBA**

Akiwa mjini Wilmington, Delaware, Rais Mteule Joe Biden aliahirisha hotuba yake wakati akizungumzia masuala ya uchumi, kasha kulaani uvamizi huo na kuuita uasi.

"Saa hii demokrasia yetu iko chini ya shambulio lisilokuwa la kawaida, tofauti na kitu chochote kile tulichokiona katika nyakati za kisasa, shambulio dhidi ya ngome ya uhuru, jinge la Capitol."

Alikamilisha hotuba yake fupi kwa kumtaka Trump ajitokeze katika televisheni ya kitaifa kulaani ghasia hizo na akomeshe vurugu hizo.

Dakika chache, Trump alitoa ujumbe wake kwa taifa lakini sio kama Biden alivyopendekeza.

Badala yake, alirudia malalamiko yake kuhusu madai ya kuibiwa kura na kuwaomba wafuasi wake warudi nyumbani.

Katika jambo ambalo liliwashangaza wengi, Trump aliweka ujumbe kwenye ukurasa wa Twitter mara mbili akiwasifu wafuasi wake, lakini baadaye ziliondolewa na Twitter.

Mtandao huo uliamua kuchukua hatua isiyokuwa ya kawaida ya kufungia akaunti ya rais kwa saa 12.

Facebook na You tube pia zilichukua hatua kama hiyo haraka.

Baada ya taharuki ya mchana hadi jioni, maofisa wa polisi hatimaye walifanikiwa kudhibiti hali ya usalama katika jengo la Capitol, huku kauli za kulaani vurugu hizo zikitolewa na viongozi mbalimbali duniani.

Wanasiasa wa Chama cha Democratic, kama Senati Chuck Schumer, alimtupia lawama rais kwa tukio hilo.

"Januari 6 itakumbukwa kwa masikitiko makubwa katika historia ya Marekani," alisema.

Kasha akaendelea "Hii ni mwisho kwa nchi yetu kwa kukubali kuwa na rais wa aina hii, watu walivyomwezesha na vyombo vya habari vinavyounga mkono madai yake ya uongo na watu wanaomuunga mkono wanaingia katika jaribio la kuiweka Marekani mashakani."

Wanasiasa wa Republican pia walimgeuka Trump na kulaani kitendo hicho.

"Tumevamiwa bungeni muda mfupi uliyopita katika jaribio la kutuzuia kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba," aliandika kwenye Twitter mbunge Lynne Cheney, mkosoaji wa mara kwa mara wa kiongozi huyo.

"Bila shaka Rais alibuni kikundi hiki, alichochea kundi hili, rais alihutubia kundi hili."

Trump pia alikosolewa na washirika wake wa karibu kama vile Seneta Tom Cotton wa Arkansas, ambaye alisema.

"Wakati umewadia kwa rais kukubali matokeo ya uchaguzi, akome kuwapotosha Wamarekani na kuzuia vurugu," alisema.

Mkuu wa watumishi wa mke wa Rais, Melania Trump, Stephanie Grisham na naibu wa ofisa wa idara ya habari, Ikulu ya White House, Sarah Matthews, walijiuzulu kupinga vurugu hizo.

Kituo cha televisheni cha CBS, kiliripoti kuwa baadhi ya maofisa wa Rais Trump, wanajadili namna kutumia kifungu cha 25 cha katiba ya Marekani, ambacho kinaelezea jinsi makamu wa rais na mawaziri wanavyoweza kumwondoa rais madarakani kwa muda.

**KWA MSAADA WA MITANDAO**

# Viazi lishe vilivyoimarisha afya ya watoto wa mkulima

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**



Familia ya Mwanzalima wakifurahia viazi lishe asubuhi. **PICHA: MARCO MADUHU.**

UDUMAVU wa watoto wadogo mkoani Shinyanga unachangiwa na wananchi kutokuwa na elimu ya lishe bora, kutokujua ni vyakula gani sahihi vya kuwapatia watoto tangu kutungwa mimba hadi kujifungua na katika hatua zote za ukuaji baada ya uzazi.

Shinyanga ni miongoni mwa maeneo yanayokabiliwa na kiwango cha juu cha udumavu ukifikia asilimia 32 wakati kitaifa ni asilimia 34.

Dogani Mwanzalima ni baba wa watoto saba mkazi wa Kijiji cha Negezi kilichoko wilayani Kishapu anayesimulia manufaa aliyopata kutokana na kupokea elimu ya kulima viazi lishe namna ilivyomsaidia kuimarisha afya za watoto wake, na hasa mtoto wa mwisho ambaye alizaliwa akiwa na udumavu.

Anasema watoto wake hao saba afya zao zilikuwa si za kuridhisha na hasa mtoto wa mwisho ambaye alizaliwa akiwa na udumavu, lakini baada ya kuanza kula viazi lishe sasa hivi afya za wanawe zimeimarika.

Anasema alipewa elimu hiyo ya kulima viazi lishe mwaka juzi (2019) akalima robo heka na baada ya kuona faida yake ndipo mwaka jana (2020) akapanua wigo na kulima hekari saba ili kula vyumbani na baadhi kuviuza ili apate pesa ya mahitaji.

"Kilimo hiki cha viazi lishe ni kizuri kimekomboa afya za watoto wangu na sita kiacha katika msimu wa mavuno uliopita nilitengeneza michembe ya viazi lishe, na viazi vingine kuvihifadhi sehemu salama, ndiyo naendelea kuvila kwa sasa huku nikisubiri mavuno mengine ambayo nimelima," anaongeza.

Milembe Kulwa ni mke wa Dogani Mwanzalima, anasema elimu hiyo ya viazi lishe pia wamekuwa wakiitoa kwa majirani zao, ili kuokoa afya za watoto wao kwa kula viazi hivyo vya lishe.

"Wanawake wenzangu wamekuwa wakiniuliza mambo mengi na hasa kuhusu afya za watoto wangu kuimarika nami nawajibu tunatumia chakula cha viazi lishe na vingine ndiyo maana wananenepa, wananiomba mbegu nami nawapatia viazi lishe ili na wao wakalime na kuwapatia.

Mhudumu wa afya ya mama na mtoto ngazi ya jamii Mary Nyanda, anasema wamekuwa wakitoa elimu ya lishe kwa wananchi kwenye kata hiyo ya Ukenyenge, pamoja na umuhimu wa kunyonyesha watoto maziwa ya mama ili kuondokana na tatizo la udumavu.

Anasema kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2020/2021 wananchi wameitikia sana kulima kilimo hicho cha viazi lishe tofauti na mwaka jana baada ya kuona familia zilizolima viazi hivyo afya za watoto wao zimeimarika na kuwa na afya njema.

"Elimu hii ya viazi lishe tumekuwa tukiitoa kwa wananchi pamoja na kwenye vikundi vya akina mama, na kisha kuwapatia mbegu za viazi lishe kwa ufadhili wa Shirika la WorldVision, ambapo pia tuna waambia wahifadhi mbegu hizo ili kilimo kiwe endelevu na siyo kutegemea misaada," anasema Nyanda.

Mkurugenzi wa miradi kutoka Shirika la World Vision, Nesserian Mollel, anasema wanatekeleza mradi wa lishe (ENRICH) katika wilaya 36 hapa nchini ikiwamo wilaya ya Kishapu, ambapo wamekuwa wakitoa elimu ya lishe kwa wananchi, pamoja na kulima viazi lishe na kuwapatia mbegu za zao hilo.

Anasema ni miaka mitano sasa wamekuwa wakitekeleza mradi huo wa lishe, ambapo kwa jamii ambayo imeshapata elimu hiyo tayari kuna mafanikio ya kubadili afya za watoto wao, hasa ile jamii ambayo ina uwezo wa hali ya chini kimaisha.

"Shirika la World Vision tunatekeleza mradi huu wa lishe (ENRICH) takribani miaka mitano sasa na bado jamii inahitaji kupewa elimu ya lishe zaidi, licha ya kuwapo na mafanikio kwa baadhi ya kaya ambazo zimeshapata elimu hiyo na sisi tutaendelea kushirikiana na serikali hadi kulimaliza tatizo la udumavu kwa watoto," anasema Mollel.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa huduma za lishe kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Grace Moshi, anasema tatizo la udumavu ni matokeo ya ukosefu wa elimu ya lishe kwa wazazi hasa waishio maeneo ya vijijini ambao wanaishi kwa mazoea.

Anaeleza kuwa vinaongeza vitamin A na kupandisha kwa kasi kinga ya mwili ambayo ndiyo nguvu ya kupambana na maradhi.

Anasema elimu ya lishe inahitajika sana kwa wananchi pamoja na kuzingatia makundi matano ya chakula, hasa katika maeneo hayo ya vijijini ambapo hawazingatii ulaji vyakula bora na hawajui ni chakula gani mtoto ana paswa kupewa na kipi asipewe, bali wao kila chakula ni halali kwa mtoto.

"Elimu hii ya lishe ikitolewa kikamilifu wizara ya afya kitengo cha lishe, tuna amini tatizo la udumavu kwa watoto hapa nchini hadi kufikia 2025 litakuwa limepungua kwa kiasi kikubwa," anasema Moshi.

Ofisa lishe Mkoa wa Shinyanga, Dennis Madeleke, anasema wanaendelea kutoa elimu ya lishe bora kwa wananchi mkoani humo kwa kushirikiana pia na mashirika mbalimbali, ili kuhakikisha hali ya udumavu kwa watoto iliyopo kwa sasa ya asilimia 32 inapunguzwa.

"Serikali kwa kushirikiana na Shirika la World Vision hivi karibuni tumezindua kitengo cha kutoa huduma za lishe kwenye hospitali ya mkoa wa Shinyanga, ambapo ni moja ya jitihada ambazo tunaonyesha za kupambana na tatizo la udumavu," anasema Madeleke.

Aidha, anatoa wito kwa wazazi mkoani humo, kutumia elimu hiyo ya lishe ambayo wanaipata kuitekeleza kwa vitendo na siyo kupuuzia, kwa sababu ni njia bora ya kukuza watoto wao wasipate magonjwa na kuwa na afya bora.

HABARI KIMATAIFA

## Mipira ya kiume yaleta utata Zambia

**LUSAKA,** Zambia

MBUNGE mmoja wa Zambia ameituhumu serikali kusambaza mipira ya kiume isiyo na ubora na kufananisha hatua hiyo sawa na mauaji ya kimbari.

Mbunge huyo Mwansa Mbulakulima, alisema usambazi wa mipira hiyo na glavu ambayo haina viwango vya usalama vinasababisha mauaji kwa watu wanaoitumia.

"Kile ambacho wizara ya afya inakifanya ni mauaji ya kimbari," Mbulakulima aliiambia BBC.

Alisema unapoweka maji katika glavu na mipira hiyo ya kiume inavuja, kitu ambacho kinatia wasiwasi watu wangapi wamefariki kuanzia mwezi Septemba kutokana na uzembe huo.

Mbunge huyo aliendа mbali kwa kuonyesha wasiwasi wake kuhusu usambazaji wa vifaa vya kujikinga na virusi vya corona kama vina usalama.

Mbulakulima na wenzake katika kamati ya bunge walisikitika kutokana na kampuni ya Honey Bee, kupewa kandarasi ya kusambaza mipira ya kondomu na glavu ambayo ina hitilafu.

Mkurugenzi Imran Lunat, aliishutumu ofisi ya mkaguzi mkuu kwa kuwa na upendeleo katika ripoti yake ambayo ilibaini kampuni hiyo haina ofisi ya moja kwa moja, kulingana na ripoti ya gazeti la serikali Daily Mail.

Ukaguzi huo pia ulibaini zabuni hiyo ilitolewa Jumapili ambayo sio siku rasmi ya kazi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Kakulubelwa Mulalelo, aliiambia kamati hiyo kuwa hafahamu ni nani aliruhusu kutolewa kwa zabuni hiyo, na kwamba yeye alihudhuria uzinduzi na usambazaji wa bidhaa hizo pekee. **BBC**

## Mnangagwa ainanga Marekani

**HARARE,** Marekani

RAIS wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, amezungumzia vurugu zilizotokea Marekani baada ya wafuasi wa Rais Donald Trump kuvamia jengo la bunge Capitol Hill, akisema nchi hiyo haina haki ya kuadhibu zingine kimaadili.

Rais Mnangagwa aliandika ujumbe kwenye mtandao wa Twitter, akiiambia Marekani haina haki ya kimaadili kuadhibu nchi zingine kwa misingi ya demokrasia. Alisema kuwa Marekani imeiwekea Zimbabwe vikwazo vikali vya kiuchumi katika misingi ya kukiuka haki ya kidemokrasia.

Ujumbe wa kiongozi huyo uliongeza "Zimbabwe iko na imekuwa tayari ushirikiano wake kama marafiki na washirika wa Marekani kwa manufaa ya nchi zote mbili."

Marekani na Umoja wa Ulaya zote zimeendeleza vikwazo vyao dhidi ya Zimbabwe kwa madai ya ukosefu wa demokrasia endelevu, ukandamizaji wa haki za binadamu pamoja na kubanwa kwa vyombo vya habari. **BBC**

# Hatimaye Trump akubali kukabidhi madaraka

**WASHINGTON,** Marekani

SIKU chache baada ya tukio la waandamanaji wanaomuunga mkono kuvamia na kushambulia jengo la bunge, hatimaye Rais wa Marekani Donald Trump, amekubali kuachilia madaraka kwa amani.

Katika taarifa yake aliyoitoa jana, kiongozi huyo alilaani shambulio hilo na kuliita baya na kueleza yupo tayari kuanza mchakato wa makabidhiano ya madaraka ifikapo Januari 20 kwa amani.

Akitumia ukurasa wake wa Twitter, saa chache baada ya kurudishwa katika mtandao wa twitter kufuatia kufungiwa kwa kipindi cha saa 12, kiongozi huyo kutoka chama cha Republican, alionekana kuachana na madai yake ya kuibiwa kura.

Hata hivyo, baadhi ya viongozi wa Chama cha Democrat, wameanza utaratibu wa kumwondoa madarakani kabla ya kumaliza muda wake wa siku 13 alizosalia madarakani.

**Wakati wa mkutano wake wa juzi, aliwaambia wafuasi hao kuelekea katika jumba la Capitol Hill, ambapo waliingia ndani kwa lazima.**

Wakati wa mkutano wake wa juzi, aliwaambia wafuasi hao kuelekea katika jumba la Capitol Hill, ambapo waliingia ndani kwa lazima.

Matamshi hayo ya Rais Trump, yalionekana kwa mara yake ya kwanza kukubali hadharani kwamba alishindwa katika uchaguzi wa mwezi Novemba.

Trump aliandika katika akaunti yake ya twitter Alhamisi jioni, alisema sasa bunge la Congress limeidhinisha matokeo na utawala mpya utaingia tarehe 20 Januari.

Alisema lengo lake ni kuhakikisha mchakato wa kukabidhi madaraka unafanyika kwa njia ya amani.

"Wakati huu tunahitaji maridhiano."

Pia aliwapongeza wafuasi wake na kuwaahidi kwamba safari yao ndio imeanza. Katika upande mwingine, Polisi wamekosolewa kwa namna walivyoshughulikia ghasia hizo.

Picha zilizonaswa ndani ya bunge zilionesha baadhi ya waandamanaji walivyokuwa wanaingia katika vyumba vya bunge bila kuzuiliwa na yeyote.

Mtu mmoja alionekana akiingia katika ofisi ya Spika Pelosi na kuweka muguu yake juu ya meza yake.

Kufuatia tukio hilo, mkuu wa polisi alipewa likizo ya lazima baada ya mwanamke mmoja kupigwa risasi na kufariki dunia akiwa kwenye sakafu ya ukumbi wa bunge la wawakilishi.

Mwanamke huyo inasemekana alikuwa mwanajeshi. Shirika la Ujasusi linatafuta waliohusika na uvamizi huo na pia wizara ya sheria ilisema waliokamatwa huenda wakakabiliwa na makosa manne.

Polisi ilisema watu watatu Benjamin Philips (50) kutoka Pennsylvania; Kevin Greeson (55), kutoka Alabama na Rosanne Boyland (34) wa Georgia. **BBC**



Askari wa Magereza wakimsindikiza kiongozi wa dini ya Kiislam, Abu Bakar Bashir, baada ya kuachiwa huru kutoka Gereza la Gunung Sindur alikokuwa akitumikia kifungo kwa kuhusika na shambulio la bomu mwaka 2002. **PICHA: AFP**

# Vikosi vya Eritrea viliingia Tigray

**ADIS ABABA,** Ethiopia

JESHI la Ethiopia limedai vikosi vya Eritrea viliingia kwenye ardhi yake bila kupewa ruhusa wakati askari wa serikali wakipambana na waasi katika mkoa wa Tigray. Jenerali mmoja alinukuliwa akisema hayo katika mkanda wa video uliorushwa kwenye mitandao ya kijamii wiki hii. Katika video huyo ambayo haijaweza kuthibitishwa na shirika la habari la Reuters, unamwonyesha Meja Jenerali Belay Seyoum, akiongoza mkutano katika mji mkuu wa Tigray, Mekelle, mwishoni mwa mwezi Desemba. Matamshi ya Jenerali huyo yanaweza kuyashtua mataifa washirika ya Magharibi ambayo yana wasiwasi kwamba uvamizi kama huo utaweza kuchochea mzozo katika mkoa wa Tigray ambao tayari maelfu ya watu wamefariki dunia.

Ethiopia na Eritrea zilisaini mkataba wa amani mwaka 2018 wa kumaliza miongo miwili ya uhasama. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**OFISI ZA MATANGAZO**
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

## KUPOTEA KWA CHETI



Ndugu **JAMES MORUMBE** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S/0880/0046** kilichotolea na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **KAIGARA** mwaka **2003**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi **Polisi taarifa IAB/RB/894/2020**

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**JOSEPHINA MAYUKI** AMBAYE NI MLEZI WA **CHARLES MAYUKI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFA YA KIWANJA **NAMBA 1299/ A KITALU "GG" (HD)** KITANGILI MANISPAA YA SHINYANGA.
KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA **JOSEPHINA MAYUKI** KWA SIMU NAMBA **0755-855162** AU **0653-315842**
**RB NAMBA SHY/RB/2020/ CONTROL NAMBA 9910819023832.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**KHALIFA RAMADHANI LALY** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** Yenye namba za usajili **MC 251 BPS.**Chassis No. **MD2A21BZ4GW193139**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DOM/RB/7487/2021.**

## IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT SONGEA
## LAND APPEAL NO 1 OF 2020

(from the decision of the district land and housing triburnal of SONGEA district in land appeal /application no 18 of 2017 and original ward triburnal of – ward **ROMWARD MAURUS MBIUNYI** applicant

Versus

**SERIKALI YA KIJIJI CHA ITWANGO AND 7 OTHERS RESPONDENT TO ERNEST FUJJI**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

Take an notice the above case have been fixed for healing on 11th February 2021 at 9:00 am before hon I.Arujani JUDGE . you are required to appear in this court on the fixed date without fail.
Order and the seal of the court this 17th day of November 2020

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA
## (MCA/63)
## Mahakama ya mwanzo ya TUNDUMA
## Wilaya ya MOMBA

**MADAI NAMBARI 04 YA 2021**
Mdai **ALEX MICHAEL MWAMBELE**
Amdai
Mdaiwa **LUCAS SIMBEYE** kwa **LUCAS SIMBEYE**
Kwakua mdai/wadaiwa ameleta madai yake kwamba
Madai ya fedha tsh 7,000,000 millioni saba

Kwahiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 21/01/2021 saa 2:30 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwakua siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri lako hilo,ni lazima kuleta mshahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalau kama hukuhudhuria /hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kwitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 06/01/2021




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SOLSKJAER ATOA NENO KUTOLEWA CARABAO




**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, ametoa sababu baada ya timu yake kupoteza mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la Carabao mbele ya Manchester City kwa kufungwa mabao 2-0.

Solskjaer amebainisha kwamba, wachezaji wake walicheza vizuri, lakini hawakutumia vvyema kila nafasi waliyoipata kwenye mchezo huo na matokeo yake wakajikuta wakipoteza.

"Wachezaji wamecheza vizuri, wamelinda vizuri ila walishindwa kutumia nafasi ambazo wamezitengeneza," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari. "Tumecheza dhidi ya timu bora ya Manchester City.

Mabao ya City ndani ya Uwanja wa Old Trafford yalifungwa na John Stones dakika ya 50 na Fernandinho dakika 83.

Ndani ya dakika 90, City ya Pep Guardiola iliweza kutawala mchezo huo kwa asilimia 61, huku United ikiwa na asilimia 39 ndani ya dakika hizo.

Pia United ilipiga jumla ya mashuti mawili yaliyolenga lango huku Manchester City ikipiga jumla ya mashuti manne ambayo yalilenga lango.

Ushindi wa Manchester City unaifanya iweze kupenya hatua ya fainali na itakutana na Spurs ya Jose Mourinho.

# Klopp aeleza hatasajili mlinzi

**LIVERPOOL,** England


KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema klabu hiyo haina mpango wa kumsajili beki wa kati katika dirisha hili dogo la usajili licha ya kwamba ina uhitaji wa mlinzi wa kati.

Klopp amesema sababu kubwa ambayo imepelekea kutosajili kuwa ni anguko la uchumi ambalo klabu hiyo inakabiliwa nalo lililochagizwa na janga la virusi vya corona.

Walinzi Virgil Van Dijk na Joe Gomez wote wako nje ya uwanja kwa msimu mzima wakati huo huo Joel Matip amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya hapa na pale tangia mwaka 2016.

"Hili ni tatizo kwetu wote, ingawa baadhi ya klabu zinaweza zikawa sawa," alisemsa Klopp akinukuliwa na Sky Sport.

Kwa ujumla msimu huu Liverpool imekuwa ikicheza bila mlinzi asilia kutokana na majeruhi kwa wachezaji wengi wa eneo la beki, ambapo katika mchezo dhidi ya Southampton alianza Jordan Henderson na Fabinho, hata hivyo bado ni vinara wa Ligi Kuu England.







# *Morata kurejea dhidi ya Inter*

**TURIN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Alvaro Morata, anaendelea vizuri na anatarajia kuwa fiti kurejea dimbani kwenye mechi dhidi ya Inter Milan.

Mchezo huo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, unatarajiwa kupigwa ifikapo Januari 17, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Sky Sport Italia, nyota huyu raia wa Hispania anaendelea vizuri kwa sasa baada ya kukosa mechi dhidi ya Udinese na AC Milan kwa sababu ya kuuguza jeraha la misuli.

Nyota huyu bado hatakuwa tayari kwenye mechi ya wikiendi hii dhidi ya Sassuolo, lakini anatarajiwa kuwa atarejea benchi kwenye raundi ya 16 ya Copa Italia kwenye mechi dhidi ya Genoa hapo Januari 13, mwaka huu.

Kama Morata ataweza kufanya vyema kwenye mechi hii basi anatarajiwa kuwa atakuwapo kwenye kikosi kitakachoanza dhidi ya Inter.

Baada ya mechi hiyo Juventus watakuwa na kibarua kingine siku tatu baadaye kwenye Supercup dhidi ya Napoli utakaochezwa Januari 20, mwaka huu.

## HABARI MICHEZO



# DIALLO ATUA RASMI MAN UTD

**MANCHESTER,** England

HABARI njema kwa mashabiki wa Manchester United ni kwamba, Amad Diallo ametua rasmi kwenye kikosi cha timu hiyo.

Diallo alisajiliwa na United mwishoni mwa Oktoba, lakini kutokana na taratibu za usajili kutokukamilika kwa muda, aliendelea kubaki katika timu yake ya Atalanta ya nchini Italia wakati utaratibu wa kukamilisha usajili ukiendelea.

Baada ya kupatiwa nyaraka muhimu za kumtambua kama mchezaji halali wa Mashetani Wekundu hao, klabu hiyo imemtangaza rasmi mchezaji huyo na punde atajiunga na wachezaji wengine muda mfupi baada ya kupatiwa vibali vyote.

Akiwa Atalanta, Diallo amecheza michezo mitano ya kikosi cha kwanza akiwa amepachika bao moja pekee.

Uwezo wake uwanjani unamfanya kinda huyu kufananishwa na Lionel Messi akiwa na umri wa miaka 18 kwa sasa.

Diallo amesaini mkataba wa miaka mitano ambao unaweza kuongezwa mwaka mmoja wa ziada na huenda akapatiwa nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza chini ya Ole Gunnar Solskjaer.

## Dortmund yakanusha Brandt kwenda Arsenal

**DORTMUND,** Ujerumani

MKURUGENZI wa Michezo wa Borussia Dortmund, Michael Zorc amesisitiza hakuna "ofa yoyote" kwa mchezaji wao anayetajwa kuwaniwa na Arsenal, Julian Brandt.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia kwenye Ligi Kuu England wakati huu wa dirisha la usajili la Januari.

Lakini Zorc amesema hakuna ofa yoyote iliyowasilishwa mezani kwao kwa ajili ya kiungo huyo, ambaye mkataba wake wa sasa na Dortmund unamalizika ifikapo mwaka 2024.

Sitaki kujibu swali lolote la uvumi ambao unatengenezwa na vyombo vya habari.

"Kila siku nasoma kwamba Brandt anawaniwa na klabu fulani, lakini sisi hatujapata ofa yoyote hadi sasa," alisema akiwaambia waandishi wa habari. "Kwa sasa tunatambua kwamba yeye ni mchezaji wetu, hizo habari anawania na klabu nyingine sisi hatujui kabisa."





## Mkataba wa Lacazette wapigwa kalenda

**LONDON,** England

ARSENAL imepanga kusubiri hadi mwishoni mwa msimu kuanza mazungumzo na mshambuliaji wake, kwa ajili ya kumwongezea mkataba mpya.

Mkataba wa sasa wa Arsenal na Lacazette umebakiza miezi 18 na ilionekana kama timu hiyo ingeanza sasa harakati za kumpa mkataba mpya, lakini imeamua kuuchuna kwa muda hadi wakati wa usajili wa majira ya kiangazi utakapofika.

"Hatujazungumza chochote kuhusiana na mkataba wake. Tutazungumza wakati wa kiangazi na kutoa uamuzi wa nini kitatokea," amesema Arteta akinukuliwa na Sky Sport.

"Ninafurahishwa na jinsi anavyocheza, mabao anayofunga na kiwango alichonacho kwa sasa. Anatakiwa kuendelea kufanya hivyo," alisema Arteta.

Lacazette katika mechi tatu za hivi karibuni amekuwa na kiwango bora zaidi huku akifunga kwenye mechi zote tatu zilizopita.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AFUNGUKA HATIMA YA OZIL

Tayari klabu mbalimbali zamwania Mjerumani huyo ikiwamo vigogo wa Uturuki, Fenerbahce...

**LONDON,** England

HATIMA ya Mesut Ozil ndani ya Arsenal itajulikana "siku chache zijazo", huku uamuzi juu ya majaliwa yake ukitarajiwa kuchukuliwa haraka hivi karibuni, kwa mujibu wa Mikel Arteta.

Ripoti za hivi karibuni zilibainisha Ozil alifanya mazungumzo na klabu ya Ligi Kuu Marekani, MLS, DC United na miamba ya Uturuki, Fenerbahce, ambayo ni timu inayotajwa kuwa inashabikiwa na nyota huyo wa zamani wa Real Madrid tangu akiwa mtoto.

Ozil alijiunga na Arsenal kutoka Los Blancos mwaka 2013 na ametoa pasi za mwisho 54 katika mechi 184 za Ligi Kuu England, huku Kevin De Bruyne (74), David Silva (63) na Christian Eriksen (62) ambao ndio wamemzidi raia huyo wa Ujerumani.

**Hata hivyo, alianza mechi mbili tu kwa msimu wa 2019-20, wakati akiwa hana namba kwenye kikosi cha Arteta.**

Huku mkataba wake ukikaribia kufikia mwishoni mwa msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 sasa yupo huru kufanya mazungumzo na klabu yoyote kuhusu uhamisho wake.

Ripoti za nchini Uturuki zinadai kwamba, tayari dili limeshafikiwa na Fenerbahce huku Arteta akikataa kusema chochote na kuahidi uamuzi utachukuliwa haraka hivi karibuni.

"Sijui nini kitatokea," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari juzi Alhamisi.

"Kwa sasa yupo huru kufanya mazungumzo na klabu yoyote, sisi tutajadiliana ndani ya klabu kuhusu hali yake na majaliwa yake.

"Kila mchezaji anataka kucheza soka, ndio maana tunasajili wachezaji kwa mikataba.

"Tunabahati kufanya kile tunachokifanya sasa, hivyo kila mchezaji anataka kucheza, lakini ni ngumu kwa kila mchezaji kupata nafasi.

"Tutaamua nini kitatokea siku chake zijazo."

## ZISIKUPITE

### CITY KUMSAJILI MESSI

KLABU ya Manchester City inakaribia kumsajili 'Messi mdogo' Dario Sarmiento. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 na winga wa Argentina anaichezea klabu ya Estudiantes katika ligi ya nchi hiyo. ***(Talksport)***

### MWELEKEO WA OZIL

KOCHA wa klabu ya Fernabahce, Erol Bulut, amesema mwelekeo kuhusu uwezekano wa klabu hiyo kumsajili kiungo mchezeshaji wa Arsenal na Mjerumani, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32 itakuwa wazi katika siku chache zijazo. ***(Mirror)***

### NEWCASTLE KUJIIMARISHA

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce anataka klabu hiyo kusajili wachezaji watatu wa England wanaoichezea Manchester United kwa mkopo mwezi huu na huku akiweka wazi pia kumhitaji winga, Brandon Williams, 20, beki Phil Jones miaka 28, na kiungo Jesse Lingard (28). ***(90min)***

### SEDIBE ANUKIA EPL

KLABU ya Newcastle imewasiliana na Monaco kuhusu beki wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Djibril Sidibe mwenye umri wa miaka 28. ***(Foot Mercato)***

### DYCHE AITAJA CORONA

KOCHA wa Burnley, Sean Dyche ametaka chanjo ya corona kuharakishwa katika soka, huku fedha zinazohifadhiwa kwa ajili ya kuwapima wachezaji zipelekwa katika idara ya afya. ***(Guardian)***

### DE BEEK KUONDOKA

KIUNGO wa Manchester United na Uholanzi, Donny van de Beek (23), huenda akaondoka kulingana na mshambuliaji wa zamani wa klabu hiyo, Dimitar Berbatov. Mchezaji huyo ameanzishwa katika mechi mbili tu za Ligi Kuu England msimu huu baada ya kusainiwa kwa dau la pauni milioni 35 hapo Septemba, mwaka jana. ***(Betfair via Sun)***

### ROMERO KUREJEA DIMBANI

GOLIKIPA wa Manchester United na Argentina, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 33, anatarajiwa kurudi katika klabu hiyo wiki ijayo huku mazungumzo kuhusu hatima yake yakiendelea. ***(Sky Sports)***

### MESSI, NEYMAR WATETA

LIONEL Messi, 33, amemwambia Neymar anapanga kuondoka Barcelona kipindi cha majira ya joto kijacho na kujiunga Paris St-Germain, huku straika huyo wa Argentina akiwa anawaniwa na Manchester City. ***(Star)***

### SABITZER ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa RB Leipzig, Marcel Sabitzer mwenye umri wa miaka 26, lakini usajili huo hautafanyika mwezi huu. ***(Express)***

### ELMOHAMADY HAKIJAELEWEKA

KLABU ya Al Ahly ya nchini Misri imeondoa uwezekano wa kumsajili mlinzi wa pembeni wa Aston Villa, Ahmed Elmohamady mwenye umri wa miaka 33. ***(Birmingham Live)***

## Azam yatamba italinda rekodi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kuanza kwa matokeo ya sare, Kocha Mkuu wa Azam FC, George Lwandamina, amesema rekodi ya timu hiyo kufanya vizuri katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi itaendelea kubaki.

Azam FC ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi Mlandege ya Kisiwani Unguja katika mechi yake ya kwanza ya hatua ya makundi iliyochezwa juzi usiku.

Lwandamina alisema anajipanga kufanya vizuri katika mechi inayofuata ili wasonge mbele na hatimaye kuibakisha rekodi nzuri waliyonayo kwenye mashindano hayo. Kocha huyo alisema mechi hiyo ilikuwa ngumu na wachezaji wake walijitahidi kucheza vizuri katika dakika zote 90 za mchezo huo, lakini wapinzani wao nao walijipanga kuwazuia.

Naye Kocha Mkuu wa Mlandege, Ali Omar, alisema wachezaji wake walijitahidi kupambana licha ya kutokuwa na ratiba rafiki katika mashindano hayo.

"Wachezaji walijitahidi kupambana licha ya uchovu kwa kucheza mechi mbili mfululizo, na mechi zote zilikuwa ngumu, hivyo kwa matokeo ya jana (juzi), wanastahili pongezi," alisema Omar.

Katika mechi hiyo Azam FC ndio ilikuwa ya kwanza kupachika bao kupitia mchezaji wake mpya, Mpiana Monzinzi dakika ya 32 huku Mlandege wakisawazisha bao hilo jioni dakika ya 88 kupitia kwa nyota wake, Rashid Abdallah.

## Kwaheri Anna Bayi, kuzikwa leo

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Anna Bayi ambaye alifariki dunia Jumatano wiki hii anatarajiwa kuzikwa leo kwenye eneo la familia yake lililoko Kibaha Mkuza mkoani Pwani, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mtoto wa marehemu, Sanka Bayi, alisema ibada ya mazishi itafanyika kwenye kanisa la KKKT, Mkuza kuanzia saa 5:00 asubuhi na kuendelea na taratibu nyingine za kumpumzisha mama yao.

"Mwili utatolewa hospitali kuja nyumbani leo (jana) na utalala hapo, Jumamosi (leo), utapelekwa kanisani kwa ajili ya ibada, halafu utarudi nyumbani kwa ajili ya mazishi ambayo yatafanyika hapa hapa nyumbani," alisema Sanka.

Naye Mwenyekiti wa Chaneta, Devotha Marwa, alisema wamepokea kwa masikitiko taarifa za msiba huo wa Anna ambaye alikuwa ni mdau mkubwa katika mchezo huo wa netiboli.

"Ni msiba mkubwa sana kwa CHANETA, kwetu maana kabla ya kufikiwa na umauti alikuwa bega kwa bega kwa kutoa ushauri kuhusu kuendeleza mchezo wetu, mbaya zaidi kwetu hatutaweza kuwahi mazishi yake kwa sababu tutakuwa safarini kurejea Dar es Salaam," alisema Devotha.

Aliongeza CHANETA itaendelea kumwezi Anna kwa kutekeleza kwa vitendo mipango aliyoianzia ya kukuza na kuendeleza mchezo wa netiboli.

# SERIKALI YAITA WADAU KUISAPOTI TAIFA STARS

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inafanya vyema kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Abdallah Ulega, amewataka Watanzania wote kuwekeza katika timu hiyo.

**Fainali za CHAN zinatarajiwa kufanyika kuanzia Januari 16, mwaka huu nchini Cameroon na Taifa Stars iko Kundi D pamoja na Zambia, Namibia na Guinea.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Ulega alisema hayo baada ya kukutana na viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Idara ya Michezo, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Kamati ya Saidia Stars Ishinde.

Ulega alisema serikali kwa kushirikiana na BMT, TFF, Kamati ya hamasa na wadhamini wa Taifa Stars, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), wamefungua 'milango' kwa wananchi wote kuisapoti timu hiyo ambayo inahitaji kufanya vyema kwenye mashindano mbalimbali.

Waziri huyo aliwataka mashabiki kujitokeza kuishangilia timu hiyo katika mechi yake ya kirafiki dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itakayochezwa Januari 12, mwaka huu.

"Moja ya azma kubwa tuliyojiwekea ni kufungua milango kwa Watanzania wote waweze kuisapoti Stars, kwa sababu hii ni timu ya wananchi wote, tutaweka utaratibu wa kila mmoja anayehitaji kuja kuisapoti Stars.

"Pia azimio lingine ni kuhakikisha wachezaji wote wanakamilishiwa mahitaji muhimu ikiwamo kupewa kiasi cha fedha kwa ajili ya kuacha katika familia zao, wakiwa safarini na kuepuka kuwaza mambo ya nyumbani na kwenda Cameroon wakiwa safi," alisema Ulega.

Waziri huyo pia aliwapongeza Simba na Namungo FC kwa kusonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho na kuwasisitiza Watanzania kuunga mkono pindi linapokuja suala la Taifa iwe katika ngazi ya klabu bila kujali itikadi za timu wanazoshabikia.

Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, aliishukuru serikali kwa kuungana nao kuhakikisha timu hiyo inajiandaa vyema kuelekea fainali hizo.

Naye Katibu wa Kamati ya Saidia Stars Ishinde, Hersi Said alisema: "Kwenye mchezo huu hakuna haja ya kuweka U-Simba na U-Yanga kwa sababu hili ni suala la kitaifa, tuungane kwa pamoja kuhakikisha timu yetu inafanya vizuri kwenye mchezo wa kirafiki ili ipate nguvu ya kwenda kufanya vyema huko CHAN."

Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Hamasa, Haji Manara, alisema: "Jambo la Simba limeshamalizika, kilicho mbele kwa sasa ni Taifa Stars ambayo Januari 12, mwaka huu itacheza mechi ya kirafiki, hivyo U-Simba na U-Yanga tunaweka pembeni, wote tunashika silaha moja kwa ajili ya Stars."



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Leila Mohamed Mussa (mwenye miwani), akimkabidhi kombe la ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa wanawake, nahodha wa timu ya New Generation, Mwajuma Abdallah. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# *Mwameja ataka Simba ijiimarishe*

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA chaguo la kwanza wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba na Timu ya Taifa ( Taifa Stars), Mohamed Mwameja ameishauri timu yake hiyo kusajili beki mmoja wa kati na kiungo mkabaji ili kuimarisha kikosi chao kinachoshiriki mashindano ya kimataifa yanayoendelea.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mwameja ambaye aliidakia Simba kwa mafanikio kuanzia mapema miaka ya 1990 hadi mwishoni, aliposajiliwa kutoka Coastal Union, alisema ameiangalia timu hiyo na kugundua inafanya makosa kadhaa kwenye upande wa ulinzi.

"Sisi tunaoangalia kwa jicho la tatu kuna mambo ambayo tunaomba tuwashauri Simba. Ni kweli mabeki, Joash Onyango na Paschal Wawa si wabaya, lakini wanatakiwa waongezewe beki mwingine wa kati mwenye uwezo na kiwango cha hali ya juu ili aje kusaidiana nao," alisema Mwameja.

Mwameja, ambaye aliifikisha Simba kwenye fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika mwaka 1993, alisema timu yake hiyo ya zamani pia ina tatizo kwenye nafasi ya kiungo mkabaji ambaye imeonekana haifanyi kazi vizuri ya kuwalinda mabeki.

Kipa huyo alitoa ushauri huo baada ya kuitazama Simba ikicheza kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya FC Patinum ya Zimbabwe ambapo wawakilishi hao wa Tanzania walipata ushindi mnono wa mabao 4-0.

Tayari Simba imeshamsajili beki mkabaji Mganda Thaddeo Lwanga na anaweza kuanza kuwatumikia mabingwa hao watetezi baada ya usajili wake kukamilika.

# Michezo

Jumamosi Januari 9, 2021

Nipashe




Arteta afunguka hatima ya Ozil UKURASA 22



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Simba: Hakuna kundi jepesi Mabingwa Afrika

## ●●● Itaanzia ugenini DRC dhidi ya AS Vita, yatoa dozi kwa Chipukizi katika Mapinduzi Cup...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba imepangwa Kundi A pamoja na vigogo Al Ahly ya Misri, AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Al Merreikh ya Sudan, Kaimu Kocha Mkuu, Selemani Matola amesema timu zote zilizoingia hatua hiyo ni bora.

**Simba itacheza mechi yake ya kwanza kati ya Februari 12 na 13, mwaka huu dhidi ya AS Vita halafu itarejea nyumbani kuwakaribisha Al Ahly Februari 23, mwaka huu halafu itaelekea Khartoum kuwafuta Al Merreikh kati ya Machi 5 na 6 huku ikiwakaribisha Waarabu hao jijini Dar es Salaam Machi 16, mwaka huu.**

Mechi yake ya tano itachezwa kati ya Aprili 2 na 3, mwaka huu nyumbani dhidi ya AS Vita na itamaliza hatua hiyo ya makundi kwa kuwafuata Al Ahly kati ya Aprili 9 na 10, mwaka huu.

Timu mbili zitakazofanya vyema zitatinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Akizungumza na gazeti hili jana baada ya ratiba hiyo ya makundi kutoka, Matola alisema hakuna kundi 'mchekea' na kikubwa ni timu yao kujiandaa vyema na mechi hizo na anaamini wanayo nafasi ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Matola alisema kikosi chao kilikuwa tayari kukutana na timu yoyote baada ya kutinga hatua hiyo na wanafahamu uzoefu waliokuwa nao utawasaidia kufanya vyema zaidi msimu huu.

Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mulamu Nghambi, aliliambia gazeti hili timu zote 16 zilizofika hatua hiyo ni ngumu na wao watajiimarisha zaidi kuhakikisha wanacheza hatua inayofuata.

"Hakuna kundi jepesi, timu zote 16 zilizofika hatua hii ni mabingwa wa nchi zao, ni timu bora, kila mmoja alikuwa anawaza atapangwa na nani ili ajipange atakavyokwenda kumkabili, sisi pia tutafanya hivyo hivyo," alisema Nghambi.

Aliitaja El Merreikh kuwa ni timu ambayo haijawahi kuwafunga na hivyo watahakikisha wanaiendeleza rekodi waliyonayo kila wanapokutana na Waarabu hao wa Sudan.

Wakati huo huo, Namungo FC imepangwa kukutana na CD 1 de Agosto ya Angola katika mechi ya hatua ya mtoano ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika na itaanzia hatua hiyo ugenini kati ya Februari 12 na 13, mwaka huu.

### YAANZA VYEMA MAPINDUZI

Mabao mawili ya winga Miraji Athumani na moja la Meddie Kagere, yaliiwezesha timu ya Simba kuanza vyema michuano ya Kombe la Mapinduzi kwa kuifunga Chipukizi ya Pemba mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar jana jioni.

Simba, ambayo mwaka jana ilifika fainali ya michuano hiyo na kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa, ilishtukizwa kwa bao la dakika ya 35, lililofungwa na Fakhi Sharif lakini dakika tisa baadaye, Kagere ambaye alivaa kitambaa cha unahodha kwenye mechi hiyo, aliisawazishia Simba kwa kichwa, akiunganisha krosi ya David Kameta 'Duchu' kwenye winga ya kulia.

Mashindano hayo yataendelea tena leo kwa Simba kukutana na Mtibwa Sugar, ambayo pia ilishinda mechi yake ya kwanza na mshindi wa mchezo huo atatinga hatua ya nusu fainali moja kwa moja.

# Ntibazonkiza, Kaze wang'ara tuzo za VPL

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Mrundi Cedric Kaze, ameibuka Kocha Bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa mwezi Desemba baada ya kuiongoza timu yake kufanya vyema kwenye mechi za ligi hiyo, imeelezwa jana jijini Dar es Salaam.

Kaze ambaye alijiunga na Yanga akichukua mikoba iliyoachwa na Zlatko Krmpotic, ambaye uongozi wa klabu hiyo uliona mwenendo wa timu hauendi vyema na hivyo kufanya uamuzi wa kubadilisha benchi la ufundi.

Pia kiungo mpya wa vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Saido Ntibazonkiza naye alishinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Desemba kutokana na kutoa mchango mzuri kwa timu yake kwenye mechi zote alizocheza.

Ntibazonkiza ameifungia Yanga mabao manne na kutoa mchango mkubwa kwenye timu hiyo tangu alipojiunga nayo kwenye dirisha dogo la usajili.

Wakati huo huo, Kaze amesema ataendelea kukifanyia marekebisho kikosi cha timu hiyo ambacho jana usiku kilishuka kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar kuvaana na Namungo FC ya Lindi katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Kocha huyo alisema anahitaji kuona wachezaji wake wanaimarika na kufanya vizuri kwenye michuano hiyo na baadaye kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa imara zaidi.

"Tulianza mashindano dhidi ya timu nzuri ya Jamhuri inayocheza soka safi la kuvutia, hatukutarajia kukutana na upinzani mkubwa, ila imekuwa ni somo tosha kwetu, tutaongeza umakini kwa ajili ya kuhakikisha tunafika mbali zaidi kwenye michuano hii," Kaze alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >